UKURASA 20



**Utamjuaje Pili Kitimtim?**

# DAWASA: Wananchi watakunywa maji yetu bila kuchemsha

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam



UKURASA 5

## MAISHA

Januari 10, 2021 Nipashe — Baba, Mama na Mwana — Jumapili





Ukurasa 12



Ukurasa 15 **MAISHA NI NYUMBA**

Usafi wa kitanda ni muhimu nyumbani

**Matoke ya mboga**

Ukurasa 14





UKURASA 9


Jumapili Januari 10, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0580456




## RIPOTI MAALUM

# Mambo 10 yanayomfanya Chalamila RC wa kipekee

UKURASA 4



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakiwanunulia sare na viatu vijana wao, katika maeneo tofauti jijini humo jana, kwa ajili ya maandalizi ya shule zinazofunguliwa nchini kote kesho. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri aagiza kufutwa kwa kampuni urasimishaji ardhi

UK. 2

## YALIYOMO

**UKURASA WA 5**

### WAZIRI AONA FURSA AJIRA BAHARINI

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Abdallah Hussein Kombo, ameshauri vijana wajiajiri katika biashara itokanayo na mazao ya bahari ikiwamo uvuvi wa samaki na majongoo, mwani, chumvi, mafuta na gesi.

## Silinde abaini ubadhirifu mamilioni

UKURASA 3

**MICHEZO** MAKOCHA WAZUNGU WAIGOMBEA SIMBA UK. 24

MAONI, KATUNI UK.6

# Gwajima: Simamieni maadili, weledi

**Na Catherine Sungura,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, amevitaka vyama, mabaraza na bodi za kitaaluma nchini, kudhibiti maadili na weledi katika utendaji kwa watumishi wa sekta ya afya, ili kuboresha utoaji huduma kwa wananchi.

Dk. Dorothy Gwajima alitoa agizo hilo jana wakati wa kikao na viongozi hao kwenye Ukumbi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma.

Alisema vyama, bodi na mabaraza ya kitaaluma ndiyo wasimamizi wakuu na wadhibiti wa maadili na weledi, akibainisha kuwa wananchi bado wanakutana na vikwazo vingi vya maadili na weledi wakati wakisaka huduma za afya.

"Kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ukurasa 137, imeandikwa kushirikiana na vyama vya kitaaluma vya kada ya afya katika kusimamia uzingatiaji wa maadili na weledi katika utendaji wa watumishi, hilo ndiyo tunalotekeleza," alisema.

Dk. Gwajima alisema wanapofanya ziara kwenye mikoa mbalimbali, wanakutana na kero zitokanazo na kufifia kwa maadili na weledi wa utendaji, akiagiza dosari hizo zifanyiwe kazi na yama, bodi na mabaraza ya kitaaluma.

"Ili tuweze kuhuisha hayo yote, lazima tukae pamoja na kuangalia mifumo yao ya utendaji kazi ikoje hadi unatoa mianya ya baadhi ya wanataaluma kukosa maadili na kuleta malalamiko mengi kutoka kwa wananchi," aliagiza.

Naibu Waziri, Dk. Godwin Mollel, aliwataka viongozi hao kuwajibika ili kuondoa matatizo ambayo ama wao kama mabaraza hawayaoni au yanaonwa na viongozi wa wilaya eneo husika.

"Tunakuta makosa kwenye taaluma mfano dawa zinaibiwa, lakini wewe mwenye baraza lako na unasimamia maadili hulioni hili. Hivi hujioni kwamba na wewe unatakiwa kuadhibiwa?" Dk. Mollel alihoji.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (katikati), akizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi pamoja na wakurugenzi wa Halmashauri za Mkoa wa Arusha jana, akiwa katika ziara ya kukagua utendaji kazi wa sekta hiyo mkoani humo. Kushoto kwake ni Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoa humo, Leo Komba. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Naibu Waziri ataka kufutwa mikataba kampuni urasimishaji

**Na Munir Shemweta,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameagiza kampuni za urasimishaji ambazo mikataba imekwisha na kushindwa kukamilisha kazi kwa wakati, zinyang'anywe kazi hizo na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Sambamba na hilo, ameelekeza kampuni ambazo muda wa kazi bado haujaisha zifanye kazi chini ya uangalizi ili kuhakikisha zinakamilika kwa wakati.

Dk. Mabula alitoa agizo hilo jana mkoani hapa alipozungumza na watendaji wa sekta ya ardhi na wakurugenzi wa halmashauri akiwa katika ziara yake ya siku moja kukagua utendaji kazi wa sekta hiyo na kuhamasisha ukusanyaji kodi ya pango la ardhi.

Alisema kutokana na uamuzi huo, makatibu tawala wa wilaya katika mkoa wa Arusha, watumie mamlaka yao kuunda vikosi kazi kushirikisha halmashauri ili kuharakisha urasimishaji kwenye maeneo ambayo kampuni za urasimishaji zimeshindwa kukamilisha kazi.

Awali, Dk. Mabula alisema baadhi ya kampuni za urasimishaji ardhi zimeshindwa kukamilisha kazi kwa wakati kwa visingizio mbalimbali na hata pale zilipokutana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, jijini Dar es Salaam.

Pamoja na kutoa visingizio hivyo, alisema ziliongezewa muda kukamilisha kazi lakini zilishindwa na kusababisha malalamiko kutoka kwa wananchi juu ya kazi hiyo.

"Kampuni ambazo mikataba yake imekwisha na kufikia Januari 31 hazijakamilisha kazi, zifungashe virago na kupelekwa katika vyombo vya sheria. Halmashauri zishirikiane na ofisi za ardhi za mkoa kufanya kazi hiyo," alisema Dk. Mabula.

Naibu Waziri Mabula alishangazwa na halmashauri kuweka malengo madogo katika ukusanyaji maduhuli ya serikali yatokanayo na kodi ya ardhi bila kujumuisha madeni ya wadaiwa sugu. Alisema mkoa wa Arusha wenye wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi zaidi ya 200 una madeni ya zaidi ya Sh. bilioni 178.943, lakini mkoa ulijiwekea malengo ya kukusanya Sh. bilioni 8.9 tu na kukusanya Sh. bilioni 4.2 sawa na asilimia 47 hadi Desemba, mwaka jana.

Kutokana na hali hiyo, aliwaelekeza maofisa ardhi wateule kuhakikisha wanawafikisha kwenye mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya wadaiwa wote sugu wa kodi ya pango la ardhi kwa kuwa tayari walishapelekewa ilani za madai kama sheria inavyoelekeza.

Pia alisisitiza kuwa wadaiwa wanaotaka majadiliano, wafanye hivyo ndani ya siku 14 na baada ya hapo, shauri lipelekwe kwenye baraza. Baadhi ya wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi katika jiji la Arusha ni pamoja na taasisi mbalimbali za serikali zikiwamo Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ambazo zimekubali kulipa madeni yao kwa awamu, huku Naibu Waziri akiagiza kuingia makubaliano kwa maandishi.

Halmashauri ya Jiji la Arusha pekee, inadai Sh. 4,134,610,533.23 za wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi, lakini imekusanya Sh. bilioni 2.27 sawa na asilimia 49.79 ya lengo kwa mwaka 2020/21.

# Uhaba wa saruji wakwamisha miradi

**Na Waandishi Wetu,** MWANZA

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Mwanaidi Ali Khamis, amemwagiza msimamizi wa mradi wa ujenzi wa Soko la Kisasa la Mjini Kati jijini Mwanza, kuwapo eneo la ujenzi muda wote ili mradi huo ukamilike kwa wakati.

Alitoa agizo hilo jana alipotembelea na kukagua ujenzi wa soko hilo na Kituo cha Mabasi cha Kisasa cha Nyegezi kilichoko Wilaya ya Nyamagana jijini hapo.

"Nimepata taarifa kwamba msimamizi mmoja anasimamia miradi yote miwili jambo ambalo halikubaliki na linasababisha miradi hii kuchelewa na kuna hatari itatekelezwa chini ya kiwango kutokana na kukosa usimamizi makini," alionya.

Mwanaidi alisema ni lazima msimamizi huyo awapo eneo la ujenzi saa 24 kuangalia ufanisi wa kazi, ili kupata majengo na miundombinu imara itakayosadifu juhudi za Rais John Magufuli, za kujenga miundombinu bora itakayochochea maendeleo ya wananchi.

"Kama msimamizi hakai eneo la ujenzi, basi aondolewe, awaachie wengine ambao wanaweza kufanya kazi hiyo, iwapo msimamizi hayupo, ni vema serikali ikajulishwa ili ichukue hatua stahiki bila kuchelewesha miradi," alisema.

Naibu waziri huyo alitoa siku mbili kwa uongozi wa Wilaya ya Nyamagana kuhakikisha kikwazo cha uhaba wa saruji katika miradi hiyo miwili ya kimkakati inayopewa fedha na Hazina, kinatatuliwa haraka ili kuziwezesha halmashauri kujitegemea kimapato.

Awali, mkandarasi kutoka Kampuni ya Mohamed Builders anayejenga miradi hiyo, Taher Jafferji, alilalamikia kero ya ugumu wa upatikanaji wa saruji licha ya kulipa fedha nyingi kwenye viwanda vya saruji, jambo ambalo linapunguza kasi ya ujenzi.

Alisema amepewa mkataba wa ujenzi wa miezi 18 na anatarajiwa kukamilisha ujenzi wa soko hilo Aprili mwakani, hivyo ni vema serikali ikalitafutia ufumbuzi suala la uhaba wa saruji.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dk. Phillis Nyimbi, alisema uongozi wa wilaya hiyo utahakikisha maagizo yote yaliyotolewa na Naibu Waziri, yatatekelezwa kikamilifu kwa kuwa lengo lao ni miradi hiyo ikamilike kwa wakati na kuchangia maendeleo ya Jiji na Mwanza na kutatua tatizo la uhaba wa ajira kwa wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Nyamagana, Kiomoni Kibamba, alisema mradi wa ujenzi wa soko hilo utagharimu Sh. bilioni 20.7 wakati ujenzi wa Kituo cha Mabasi Nyegezi utagharimu Sh. bilioni 15.8, sasa ukiwa umefikia asilimia nane na 10, na Wizara ya Fedha na Mipango tayari imetoa Sh. bilioni 7.13.

# Kaya 1,300 zapoteza sifa TASAF

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

UHAKIKI wa kaya za walengwa mpango wa kunusuru kaya maskini unaoratibiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) awamu ya tatu mkoani Njombe, umebaini kaya 17,475 zina sifa kuendelea kunufaika huku kaya 1,366 zikipoteza sifa na kaya 1,005 hazikuhudhuria uhakiki kutokana na sababu mbalimbali.

Akizungumza jana katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa, Mratibu wa TASAF Mkoa wa Njombe, Mussa Selemani, alisema kaya ambazo hazikuhakikiwa, zitapewa nafasi ya mwisho kuhakikiwa kabla ya kutolewa kwenye mpango ikiwa hazitajitokeza tena.

"Kikwazo kikuu kilichojitokeza wakati wa uhakiki, ni baadhi ya wakuu wa kaya za walengwa kutohudhuria uhakiki kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na baadhi ya walengwa kuwa mashambani kwa shughuli za kilimo na hivyo kutopatikana wakati wa uhakiki," alisema Selemani.

Alisema miradi mbalimbali ya sekta za maji, elimu na afya huibuliwa na vijiji vya walengwa kwa lengo la kuboresha huduma za sekta hizo kwa jamii kupitia mpango huo wa TASAF.

"Tofauti na vipengele vingine vya mpango, miradi hii haizinufaishi kaya za walengwa tu, bali kila kaya kwenye kijiji au mtaa husika ina fursa sawa ya kunufaika kupitia miradi hiyo," alisema.

Selemani alisema halmashauri za mkoa zimetekeleza jumla ya miradi 81 ikiwa ni pamoja na miradi 28 ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, ofisi za walimu na vyoo, mradi mmoja wa ujenzi wa jengo la utawala, miradi 23 ya ujenzi wa nyumba za watumishi, miradi tisa ya ujenzi wa mabweni, mradi wa ujenzi wa jengo la huduma za uzazi, miradi 17 ya ujenzi wa zahanati, mradi wa ujenzi wa jengo la kufulia na ununuzi wa mashine ya kufulia na mradi wa maji.

"Miradi hii imegharimu jumla ya Sh. bilioni 5.789 ambapo miradi 78 imekamilika na mitatu iko kwenye hatua za ukamilishaji," alisema.

Selemani alisema wanakabiliwa na tatizo la baadhi ya walengwa kushindwa kuhudumia miradi walioanzisha hasa ya ufugaji kutokana na uzee na maradhi.



Mkandarasi wa ujenzi wa kituo cha mabasi Nyegezi, wilayani Nyamagana, mkoani Mwanza, Mhandisi Taher Jafferji (wa pili kulia), akimwongoza Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mwanaidi Ali Khamis (wa tatu kulia), kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho jana, ambacho hadi kukamilika kwake kitagharimu takribani Sh. bilioni 15.8. Kushoto ni Diwani wa Nyegezi, Edith Mudogo. **PICHA: WFM**

# Waziri aagiza mkuu wa shule na wajumbe kamati wawekwe selo

**Na Thobias Mwanakatwe**

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, ameibua ubadhirifu katika ujenzi wa bwalo la Shule ya Sekondari Ikhanoda wilayani Singida, zaidi ya Sh. milioni 50 zikitumika huku ujenzi ukiwa hatua ya msingi tu.

Fedha hizo zilizotumika ni kati ya Sh. milioni 100 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa bwalo hilo uliopaswa kuanza Oktoba Mosi 2020 na ukamilike Desemba Mosi mwaka jana, lakini hadi sasa upo hatua ya msingi.

Kufuatia hali hiyo, Silinde alimvua madaraka na kumkabidhi kwa Jeshi la Polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkuu wa Shule ya Sekondari Ikhanoda, Omary Selestine, baada ya kugundua matumizi mabaya ya fedha za umma katika ujenzi wa bwalo hilo.

"Sasa, hii itakuwa fundisho kwa watu wote, huyu wala hamhitaji kuandika 'protocal' zote, huyu ninamvua madaraka hapa hapa, wala siyo kumsimamisha, ni mwizi kama wezi wengine, haiwezekani ununue tofali moja kwa bei ya Sh. 5,000 na mabati ya Sh. milioni 75," alisema.

Silinde pia alitangaza kuvunja kamati ya ujenzi ya shule hiyo na kumvua madaraka Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ikhanonda kwa kushindwa kusimamia ujenzi wa bwalo la chakula katika shule hiyo na kuhusika moja kwa moja katika ubadhirifu huo.

"OCD (Mkuu wa Polisi Wilaya) hawa wote waende ndani, hakuna mjadala, na kamati nzima wote wataandika maelezo wakiwa ndani, TAKUKURU watawachukua maelezo wakiwa ndani na hiyo bodi imevunjwa. Haya mambo ya 'protocal' ndiyo yanachelewesha mambo," aliagiza.

Silinde alisema hakuna kazi ngumu ambayo Rais anapata kama viongozi wa chini kushindwa kutekeleza wajibu wao, akiagiza baada ya wiki sita ujenzi wa bwalo hilo uwe umekamilika.

Alimwagiza Ofisa Elimu Sekondari wilayani Singida kuandika maelezo TAMISEMI kwanini asichukuliwe hatua kwa kuwa ndiye mwenye wajibu wa kusimamia miradi, lakini ameshindwa na hivyo kusababisha ubadhirifu huo.

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Pascas Muragilil, alisema Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, ilituma maofisa wa TAKUKURU kuchunguza ujenzi huo na kubaini kuna ubadhirifu wa fedha katika mradi huo na kutoa mapendekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kumsimamisha kazi mwalimu huyo.

Mkuu wa shule hiyo, Selestine alisema mpaka sasa wameshatumia Sh. milioni 57.6 kati ya Sh. milioni 100 walizopewa.

## Lukuvi afumua Idara ya Ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** CHAMWINO

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amefanya ziara ya kushtukiza katika ofisi za ardhi Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino jijini Dodoma na kuagiza kubadilishwa vituo vya kazi Mkuu wa Idara ya Ardhi, Letare Sinda, na Ofisa Mipango Miji, David Msemo.

Lukuvi amefikia uamuzi huo baada ya kukagua utunzaji wa nyaraka pamoja na maombi ya vibali vya ujenzi yaliyowasilishwa kwenye ofisi ya mipango miji kwenye halmashauri hiyo, akikerwa na ukiukwaji wa sheria na miongozo ya kutoa vibali vya ujenzi na umilikishaji ardhi ambao umechangia malalamiko ya wananchi kuongezeka. Lukuvi baada ya kuzuru ofisini huko juzi, aliagiza Kamishna wa Ardhi na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Makazi kutoka makao makuu ya wizara, watume wataalamu wengine haraka ili wakasimamie uandaaji wa nyaraka za umiliki na utoaji vibali vya ujenzi katika halmashauri ya wilaya hiyo.

Alisema Wilaya ya Chamwino ndiyo pekee ambayo ilipewa upendeleo na wizara kwa kupatiwa vifaa vya upimaji, gari la idara ya ardhi na vifa vya kompyuta lakini ndiyo wilaya inayolalamikiwa zaidi katika Mkoa wa Dodoma. "Jiji la Dodoma linakua kwa haraka sana, Wilaya ya Chamwino ndiyo wilaya namba moja na Ikulu ipo ndani yake. Ni lazima iwe wilaya ya mfano kwenye utoaji huduma za sekta ya ardhi.

"Muda wa kufanya kazi kwa mazoea hakuna tena, kila mtaalamu afuate miongozo iliyowekwa na serikali katika kutoa huduma," Lukuvi aliagiza.

Alisema Wilaya ya Chamwino imekuwa na tamaa ya kuuza viwanja kwa gharama kubwa kiasi cha kuwakatisha tamaa wananchi maskini na wanyonge ambao ndiyo wazawa wa Chamwino.

Lukuvi alisema hali hiyo inasbabisha wananchi kuyakimbia maeneo yao na kwenda kutafuta maeneo sehemu nyingine na kuanzisha makazi holela.

Aliongeza kwamba, wananchi wachache wanaoweza kununua viwanja ndani ya wilaya hiyo, bado wanakutana na kikwazo kingine cha gharama kubwa za vibali vya ujenzi. Mbali na sheria na miongozo kutokufuatwa, Waziri Lukuvi alisema maombi mengi ya vibali vya ujenzi hayajatolewa na hakuna nyaraka zinazoonyesha sababu zilizokwamisha maombi hayo.

"Haiwezekani mwananchi alete maombi ya kibali cha ujenzi yeye mwenyewe na asikifuatilie kama taratibu za utoaji huduma ni rafiki na ziko wazi," alisema.

Waziri huyo alisema kufanya kazi kwa mazoea na kutokuzingatia sheria, taratibu na kanuni katika utoaji wa huduma, kunatengeneza mianya ya rushwa na kuzalisha malalamiko ya wananchi.

Katika mwongozo wa utoaji vibali vya ujenzi uliotolewa hivi karibuni na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, wataalamu wote wanatakiwa kuweka utaratibu wa kukutana wote kwa pamoja na kupitia maombi yaliyowasilishwa ili kutoa mwanya kwa kila mtaalamu kujiridhisha na kipengele kinachomhusu. Mwongozo huo pia unawataka wataalamu hao kuhakikisha kibali cha ujenzi kinatolewa ndani ya siku saba tangu maombi yalipowasilishwa.

## MIEZI 18 NDANI YA MBEYA

# Mambo 10 yanayomfanya Chalamila RC wa kipekee

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

TAYARI ana miezi 18 au kwa lugha nyepesi mwaka mmoja na nusu, Albert Chalamila amevaa joho la Mkuu wa Mkoa wa Mbeya.

Kufika kwake kwenye mkoa huo, ambao pia una hadhi ya makao makuu ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, kuna aina fulani ya upekee katika wasifu wake, zaidi kazini na hata wakati mwingine nje ya mahali hapo.

Jicho la Nipashe mara zote lilipomwangazia akiwa kazini, ana aina fulani ya wasifu; kwanza ni mchangamfu kupitiliza na masihara ndipo mahali pake, lakini ndani ya angalizo ukivuruga, kilichomfanya Rais amteue kwenda kutumika Mbeya, utashuhudia ukali wake 'kisawasawa'.

Ndani ya masihara hayo, hufikia hatua anakosa 'breki' kuanika joto la jiwe lililomkuta nje ya ofisi na anapokuwa kikazi, tangu siku za mwanzo aliibuka na mtindo analiacha gari lake na kuingia mtaani kujumuika na 'washikaji' mbalimbali wakiwamo wadau kwenye vijiwe vya bodaboda.

Hapo wanabadilishana mawazo mawili matatu, lakini ukizama kwenye dozi yake, daima kuna darasa kwa vijana hao wakipewa kwa lugha ya 'kishikaji' na si haba anapowaaga, mkono wake unakuwa umekunja karatasi fulani ambayo pindi anapowaachia, sura yao ya tabasamu hadi jino la mwisho inakuwa bayana.

Staili hiyo ya kuvuka kwa mguu ndiyo alitumia hata kuvamia kirafiki Soko Kuu la Mwanjelwa jijini Mbeya, vivyo hivyo siku nyingine alipofika katika Hospitali ya Rufani ya Kanda jijini na kuzungumza na kirafiki kwa kina na 'wala unga' wanaolelewa katika kituo maalum.

Pia, isisahaulike, siku zake zikiwa zinahesabika tangu aanze kuanza makazi na ofisi jijini Mbeya, aliorodhesha mambo kadhaa ya kimaendeleo, lakini wahalifu aliwaanikia kwamba ni 'paka na panya' ikitilia maanani alishanong'onezwa na mafaili yanamweleza kwamba watu hao wanapatikana kwa wingi mahali hapo.

Chalamila, alivalishwa viatu vya mtangulizi wake, Amos Makalla aliyehamishiwa Mkoa wa Katavi, kupitia uteuzi wa Rais John Magufuli wa Julai 2018, akitokea Iringa, mkoa alikozaliwa, alikokuwa Mwenyekiti wa Mkoa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Yafuatayo ni mambo 10 yaliyofanywa na kiongozi huyo katika wadhifa wa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya:

**KAMATA KIJIJI KIZIMA**

Agosti 15, 2018, ikiwa ni siku chache baada ya kuanza kazi mkoani Mbeya, Chalamila aliliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata na kuwasweka ndani wananchi wote (zaidi ya 500) wa Kijiji cha Ngole kilichoko Kata ya Ilungu, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, katika moja ya mikutano yake na wafanyabiashara mkoani humo.
**PICHA: MAKTABA**

Wananchi hao walikuwa wanatuhumiwa kuhujumu miundombinu ya Mradi wa Maji wa Kijiji jirani cha Mashesye kwa kukata mabomba na kubomoa chanzo cha mradi ambao uliogharimu Sh. milioni 27.

**ACHARAZA VIKOBO WANAFUNZI**

Oktoba 3, 2019, Chalamila aliwacharaza bakora wanafunzi 14 wa Shule ya Sekondari Kiwanja wilayani Chunya ambao walikuwa wanatuhumiwa kuchoma bweni la shule hiyo kama sehemu ya kulipiza kisasi baada ya kupokwa simu walizokuwa wanamiliki kinyume cha miongozo.

Hakuishia kuwashushia bakora tu. Siku iliyofuata, alirejea tena shuleni huko na kuwatimua wanafunzi wote wa kidato cha tano na sita (walikuwa 392).

Aliwataka wanafunzi hao kurejea shuleni baada ya wiki tatu na kila mmoja kutakiwa kulipa Sh. 200,000 kwa wale ambao hawakukutwa na simu na wale waliokutwa na simu, walitakiwa warejee na Sh. 500,000.

Baada tukio hilo, kuwa na minong'ono kwamba huenda kiongozi huyo angechukuliwa hatua na Rais Magufuli, lakini ikawa kinyume cha matarajio hayo kiongozi huyo wa nchi alipojitokeza hadharani na kumpongeza kwa hatua hiyo.

Baada ya wanafunzi kutekeleza adhabu hiyo, zilikusanywa Sh. milioni 82 ambazo zilitumika kukarabati mabweni hayo mawili na kujenga bweni jipya ambalo lilipewa jina la Chalamila.

**SKIMU YA UMWAGILIAJI**

Mwaka 2018 uliisha vibaya kwa wakulima takribani 5,000 wa Skimu ya Umwagiliaji ya Mnazi iliyoko Kata ya Imalilo- Songwe wilayani Mbarali baada ya Chalamila kusimamia uvunjaji wa chanzo cha maji na kufukia mfereji wa skimu hiyo.

Shida ni nini? Alichukua uamuzi huo ili kulinda ikolojia ya Mto Ruaha baada ya maofisa wa Bonde la Maji la Mto Rufiji kudai kuwa mfereji huo ulichimbwa na wakulima hao bila kuwa na kibali na ulikuwa miongoni mwa mifereji isiyozingatia matumizi endelevu ya maji.

Siku iliyofuata, alirejea katika kata hiyo na kuwataka wakulima hao wajenge upya mfereji huo kwa maelezo kuwa Rais John Magufuli alimpigia simu na kumwelekeza awasamehe wahudumie mazao hayo kwa msimu huo pekee.

**TEMBEZA MKONG'OTO USIKU KUCHA**

Agosti 6, 2019, baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Makwale wilayani Kyela, waliushambulia kwa mawe msafara wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo na kuyaharibu baadhi ya magari likiwamo lililokuwa linatumiwa na maofisa wa usalama.

Wananchi hao walifanya tukio hilo kwa madai kuwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Cloudia Kitta, alikuwa anawatetea 'wachawi' wa kijiji hicho akiwamo mama aliyetuhumiwa kumuua mtoto wake kwa imani za kishirikina.

Tukio hilo lilimkera Chalamila, akatoa amri kwa Jeshi la Polisi kuweka kambi katika kijiji hicho na kutembeza mkong'oto kwa wananchi hao usiku kucha ili liwe fundisho kwa wananchi wengine.

Chalamila pia aliagiza wananchi hao kulipa gharama za matengenezo ya gari iliyoharibiwa.

**MSHAHARA UNATOSHA 'MCHEPUKO'**

Aprili mwaka jana, Rais Magufuli alizuru mkoani Mbeya kwa mara ya kwanza tangu alipochaguliwa kushika nafasi hiyo katika awamu yake ya kwanza.

Katika mkutano wake uliofanyika kwenye Uwanja wa CCM Ruanda Nzovwe, Chalamila alikuwa miongoni mwa wazungumzaji na alipopata fursa hiyo, alitamka maneno ambayo yalichekesha wengi.

"Mheshimiwa Rais, ninashukuru unanilipa mshahara mzuri ambao unanitosha hata kukaa na 'kamchepuko kidogo', wachungaji mnisamehe, nilikuwa ninachomekea tu," alisema Chalamila.

Maneno hayo yalionekana kutomfurahisha Rais Magufuli, japo siku hiyo hakuzungumzia chochote hadi Aprili 27 alipoendelea na ziara yake wilayani Chunya ambako pia Chalamila alitamka maneno yanayofanana na hayo.

"Mheshimiwa Rais, ninashukuru umeniletea DC (Mkuu wa Wilaya) mzuri," alisema Chalamila akimlenga Maryprisca Mahundi, sasa Naibu Waziri wa Maji.

Maneno hayo yalionyesha kumkera Rais Magufuli ambaye katika hotuba yake siku hiyo alisema amesikitishwa kutokuanzishwa kwa soko la madini wilayani huko licha ya kutoa agizo muda mrefu huku Mkuu wa Mkoa akionyesha kupenda 'michepuko'.

**KUFUFUA WAFU**

Mwaka 2019, Mkoa wa Mbeya ulikuwa miongoni mwa mikoa iliyokuwa na waganga wa jadi wengi waliotuhumiwa kupiga ramli chonganishi na kuchochea migogoro kwenye jamii, huku wananchi wakitaka serikali iruhusu shughuli hizo kuendelea.

Chalamila akiwahutubia wananchi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, alisema kama waganga hao wanataka awaruhusu kufanya kazi hiyo, wanatakiwa waende katika Chumba cha Kuhifadhia Maiti cha Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya na kufufua maiti ili waaminiwe.

Alisema kama hawawezi kufanya hivyo, hawezi kuruhusu kazi yao iendelee na akaagiza vyombo vya dola kuwashughulikia endapo watakamatwa wakifanya kazi hiyo.

**'NINAYAPENDA MAPENZI'**

Katika mikutano mbalimbali ya hadhara ambayo Chalamila amekuwa akiifanya kwenye maeneo mbalimbali mkoani humo, amekuwa akichomekea maneno ambayo yanachekesha.

Katika moja ya mikutano yake alipokuwa anazungumzia masuala ya mapenzi, alisema baadhi ya watu wamekuwa wanamtuhumu 'kupenda mapenzi', akiwajibu "kweli ninayapenda mapenzi ndiyo maana niliamua kuoa".

**WANAUME WA MBEYA**

Wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) uliandaa tamasha maalum mkoani Mbeya lililofanyika Kata ya Ijombe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Katika tamasha hilo, Chalamila alikuwa mgeni rasmi na katika hotuba yake, alisema wanaume wengi wa Mkoa wa Mbeya wanapenda kulelewa na hivyo akawashauri wanaharakati wa haki za binadamu kuliangalia jambo hilo.

**POMBE KUONDOA MAWAZO**

Katika moja ya mikutano yake na vijana wanaofanya kazi kwenye Stendi ya Mabasi Mbalizi, Chalamila aliwashauri vijana kunywa pombe baada ya kazi, akidai inaondoa mawazo.

Alitoa kauli hiyo kama masihara huku akiwataka viongozi wa dini kuacha kumpelekea kesi zinazohusu kelele za kwenye kumbi za starehe na wananchi wengine kuacha kumpelekea kesi za kelele za mahubiri kwenye maeneo yao.

**JIMBO LA SUGU LIKO WAZI**

Baada ya kuapishwa, kazi ya kwanza ambayo Chalamila aliifanya mkoani Mbeya ilikuwa ni kumwapisha Maryprisca Mahundi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Chunya, kiapo kilichofanyika Ukumbi wa Benjamin Mkapa jijini Mbeya na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa chama na serikali.

Katika shughuli hiyo, alitoa kauli ambayo ilizua hisia za watu, akisema Jimbo la Mbeya Mjini lilikuwa wazi kutokana na mbunge aliyekuwapo wakati huo, yaani Joseph Mbilinyi 'Sugu', kutokuwa na uwezo.

Kauli hiyo iliwafurahisha wafuasi wa CCM na kuzua hasira miongoni mwa wanachama na wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), chama ambacho Sugu alikuwa anakiwakilisha.

# HABARI KITAIFA



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakipita jirani na gari lililoteketea kwa moto, katika eneo Kitunda, jijini humo mwishoni mwa wiki. Hakuna mtu aliyejeruhiwa katika ajali hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## 'TEA kusanyeni madeni mliowakopesha'

**Na Christina Mwakangale**

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Kipanga Omary, ameiagiza Mamlaka ya Elimu (TEA), kuongeza kasi ya ukusanyaji madeni ya mikopo iliyokopesha taasisi hiyo, ili kunufaisha wakopaji wengine.

Ameitaka mamlaka hiyo kuwa wabunifu kwa kuandika maandiko ya maombi ya fedha za miradi, ili kuongeza vyanzo vya mapato ya kutekeleza miradi ya elimu.

Omary aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam, alipozuru kwenye ofisi za mamlaka hiyo na kukutana na watumishi na menejimenti kufahamu utendaji kazi wao.

"Nilipotembelea Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) wiki hii, nimeshangaa kuona kiasi cha Sh. bilioni 400 na zaidi walizokopeshwa wanafunzi, hazijarudi kati ya Sh. trilioni 1.2," alisema Omary.

"Bodi ya Mikopo wiki hii wananiambia zaidi ya Sh. bilioni 400 na zaidi ambazo zilikopeshwa hazijarudi kati ya Sh. trilioni 1.2, zilizokusanywa ni Sh. bilioni 800," alisema Omary.

Alisema TEA inatakiwa kuweka mikakati yakinifu ya kuzikusanya fedha za mikopo ambazo serikali ilitoa kwa ajili ya mkopo na siyo ruzuku, akisisitiza zinapaswa kurudishwa.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye, alisema hadi kufikia Desemba mwaka jana kulikuwa na deni la Sh. bilioni 5.4 ambazo mamlaka hiyo inazidai taasisi za umma na binafsi iliyozikopesha na kwamba wanaendelea kuzikusanya.

"Kuanzia mwaka 2015 taasisi za umma na binafsi 22 zilipata fedha za mkopo zilikopeshwa takriban Sh. bilioni tano," alisema Geuzye.

Alisema taasisi inakabiliana na vikwazo kadhaa ikiwamo upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi kutokana na ongezeko la mahitaji hususan katika udahili wa ngazi mbalimbali za elimu.

"Tunaandaa maandiko ambayo yatasaidia mamlaka kupata mapato ambayo yatawezesha utekelezaji wa miradi. Kwa mwaka 2020/21, tunatarajia kutekeleza miradi tofauti ikiwamo shule 116 kunufaika na miradi 123 kwenye kujengewa mabweni 13, nyumba 100 za walimu na madarasa 180," alisema Geuzye.

## Waziri aona fursa ajira baharini

**Na Christina Mwakangale,**
UNGUJA

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Abdallah Hussein Kombo, ameshauri vijana wajiajiri katika biashara itokanayo na mazao ya bahari ikiwamo uvuvi wa samaki na majongoo, mwani, chumvi, mafuta na gesi.

Amesema uchumi utokanao na bahari, hususan sekta ya uvuvi, unaweza kutoa ajira kwa vijana takribani 300,000 nchini.

Kombo aliyasema hayo jana alipofungua semina ya siku mbili kuhusu umuhimu wa sekta ya uvuvi kwa vijana wapatao 70, iliyoandaliwa na Taasisi ya Mimi na Mwinyi kwa kushirikiana na ushirika wa Wakulima Hai Co-operative Society Zanzibar.

Alisema bahari ndiyo uchumi mkuu na tegemezi wa visiwa vya Zanzibar kutokana na mazingira yake kuzungukwa na bahari na kwamba lengo la wizara hiyo mpya ni kuleta mapinduzi ya kiuchumi.

"Wizara hii ni mpya katika awamu hii ya nane, imeanzishwa na Rais Hussein Mwinyi, ikizingatiwa tumezungukwa na bahari, hivyo uchumi wa kimapinduzi utokane na fursa na mazao yatokanayo na bahari.

"Kama ilivyoelezwa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwamba uchumi wa buluu unaweza, kuajiri vijana 300,000, biashara ambayo ina mahitaji makubwa duniani hivi sasa ni majongoo ya baharini," alisema Kombo.

Waziri huyo alisema matumizi sahihi ya bahari kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira, yatasaidia vijana kujiajiri kwenye sekta ya uchumi wa buluu na watapewa ushirikiano na serikali ili kuinua vipato vyao.

"Niwahakikishie serikali itatoa ushirikiano kwa taasisi zote na wadau wanaolenga kuleta mabadiliko ya kiuchumi.

"Kwa kuanzia kongamano la vijana linalotarajia kufanyika Januari 23 mwaka huu, tutashirikiana na Taasisi ya Mimi na Mwinyi kuandaa kongamano la vijana kuelimisha ufugaji wa majongoo," alisema Kombo.

Aliongeza kuwa mkakati uliopo sasa kuhusu uchumi huo, ni utoaji elimu kuhusu mazao ya bahari kupitia vyombo vya habari.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Salmin Shukuru Botea, alisema anaungana na serikali ya awamu ya nane kuleta mapinduzi ya kiuchumi kupitia bahari.

"Hii ni fursa kwa vijana kujiajiri katika shughuli ya uvuvi wa majongoo na ufugaji ili kujiongezea kipato. Nilipoanzisha taasisi hii, lengo lilikuwa ni kukuza ajira, biashara na uchumi," alisema Botea.

Alisema wanatarajia kuanzisha ufugaji na uvunaji wa majongoo kwa kuwa ni rahisi, usiohitaji uwekezaji mkubwa kama ilivyo uvuvi wa samaki ambao unahitaji nyavu na boti ili kupata idadi kubwa. Katibu wa Ushirika wa Taasisi ya Wakulima Hai, Semeni Mohamed Salum, alisema biashara ya majongoo ilianza visiwani humo mwaka 2011 na kwamba ufugaji ulikuwa vijijini.

"Ufugaji huu una tija, serikali imeahidi sekta hii itaipa nguvu ufugaji baharini kwa kuwa mwamko ni mkubwa, waliojiajiri katika uchumi wa buluu ni wenyi, soko liko hasa Hongkong, Marekani," alisema Semeni.

## DAWASA: Wananchi watakunywa maji yetu bila ya kuyachemsha

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imewahakikishia wananchi wanaotumia maji kuwa kuanzia mwishoni mwa mwezi ujao, wanaweza kunywa maji moja kwa moja kutoka kwenye bomba bila kuyachemsha.

Hatua hiyo imekuja baada ya mamlaka hiyo kufanya kazi na chini ya Viwango vya Kimataifa (ISO).

Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Cyprian Luhemeja, alibainisha hayo juzi wakati wa ziara ya Mbunge wa Kibaha Vijijini, Michael Mwakamo, kutembelea mitambo ya kuzalisha maji ya Ruvu Juu na kuona uzalishaji wa maji katika mtambo huo.

"Ninawahakikishia wakazi wa Dar es Salaam kuwa maji ya DAWASA ni safi na salama na kwamba kwa sasa tunafanya kazi chini ya Viwango vya Kimataifa (ISO Certified), tunasubiri kuzindua cheti hicho ndani ya wiki mbili zijazo," alisema Luhemeja.

Alisema kuwa dawa ya kutibu maji na mitambo ya kisasa ya kusafisha maji ipo lakini kikwazo kikubwa ni kwa wananchi kutojiamini, akisisitiza kuwa kwa sasa wanaendelea kuziba mabomba yaliopasuka yanayopeleka maji kwa wananchi ili ikifika mwishoni mwa mwezi ujao, wananchi wapate maji salama. "Dawa zipo na mitambo ya kisasa ipo, kwa sasa tunakamilisha uzibaji wa mabomba yaliyopasuka, yanayomwanga maji kabla ya kufika kwa mteja, tukimaliza zoezi hilo, ninadhani mwishoni mwa mwezi ujao tutawatangazia wananchi kuwa kwa sasa maji ya DAWASA safi na salama," alisema.

Mbunge wa Kihaba Vijijini, Michael Mwakamo, alisema jitihada kubwa zinafanywa na serikali katika kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya majisafi na salama, hivyo wananchi wanapaswa kuwa walinzi wa miradi hiyo mikubwa.

"Nilitaka kuja kuona vyanzo vya maji wanavyotumia watu wa majimbo ya Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam, nimekutana na viongozi wa DAWASA na kunithibitishia kuwa maji haya yanayotoka hapa (Ruvu Juu) yanaweza kwenda kutumika na Watanzania ambao wanatumia maji ya mtandao wa mamlaka pasipo kuyachemsha kwani yametibiwa vizuri kwa maana ya kuyafungua tu bombani na kuyanywa bila kuchemsha," alisema Mwakamo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waliokwamisha urasimishaji wa ardhi wachukuliwe hatua

**NAIBU** Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, yuko katika ziara kwenye mikoa mbalimbali nchini kwa ajili ya kukagua utendaji katika sekta ya ardhi pamoja na kuhimiza ukusanyaji wa mapato ya serikali kupitia kodi ya pango la sekta hiyo.

Hadi jana, katika ziara hiyo, Dk. Mabula ameshatembelea mikoa ya Morogoro, Pwani, Lindi, Mtwara, Tanga, Arusha na Kilimanjaro na kukutana na madudu mbalimbali. Miongoni mwa mambo hayo ni wamiliki kushindwa kuchukua hati za ardhi, watu kushindwa kulipa kodi ya pango la ardhi.

Katika madeni ya pango la ardhi, Naibu Waziri huyo amebaini makusanyo kiduchu kulinganisha na malengo ambayo halmashauri zimejiwekea huku taasisi za serikali kama vile mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) zikidaiwa kodi za miaka mingi.

Hatua hiyo imesababisha serikali, kupitia sekta ya ardhi, kukosa fedha ambazo ama zingeendeleza sekta husika pamoja na miradi mingine ya maendeleo kulingana na bajeti ya serikali.

Licha ya matatizo hayo, Dk. Mabula pia amebaini madudu mazito katika urasimishaji ardhi ndani ya halmashauri huku baadhi ya kampuni zilizopewa mikataba ya kufanya kazi hiyo, zikishindwa kutekeleza jukumu hilo.

Miongoni mwa mikoa ambako Naibu Waziri amebaini tatizo hilo ni Kilimanjaro na Arusha, hivyo kusababisha wananchi wengi kushindwa kupata haki zao za kumiliki maeneo kwa mujibu wa sheria.

Kutokana na tatizo hilo, Dk. Mabula ameagiza kuchukuliwa kwa hatua mbalimbali dhidi ya kampuni hizo ikiwamo kufutwa kwa mikataba kwa zile ambazo zimeshindwa kufanya kazi hiyo. Miongoni mwa kampuni hizo, ni zile ambazo ziliitwa na Waziri mwenye dhamana ya ardhi na kuzungumza nazo hatimaye kupewa muda zaidi, lakini zikashindwa pia.

Wakati akiagiza kuchukuliwa hatua dhidi ya kampuni hizo, Naibu Waziri alisema licha ya kusitishiwa mikataba na kunyang'anywa, pia zinatakiwa kupelekwa katika vyombo vya sheria.

Hatua iliyotangazwa na Naibu Waziri, inaonyesha dhamira ya dhati kwamba serikali inafanya mageuzi makubwa katika sekta ya ardhi ambayo miaka nenda miaka rudi, imekuwa ikilalamikiwa na wananchi juu ya mambo mbalimbali.

Hatua ya kuwashughulikia wale waliopewa kazi ya kurasimisha ardhi, ikiwa njia mojawapo ya kumaliza migogoro ya ardhi ambayo imetamalaki nchini kote, ni ya kuungwa mkono. Kwa maneno mengine, watu walioshindwa kufanya kazi hiyo, ni wababaishaji ambao wanachafua hata sifa ya wazawa wengine wenye uwezo kupewa kazi.

Kwa miaka mingi baadhi ya kampuni za kitanzania katika sekta kama vile ujenzi, zimekuwa zikilalamikia serikali kuwa inazinyima kazi na kuwapendekeza makandarasi wa kigeni, lakini hata zinapopewa kazi, zimekuwa zikifanya chini ya kiwango au kushindwa kumaliza kwa wakati.

Ni vyema kampuni hizo na zingine ambazo hazijamaliza au kufanya kazi kama zilivyokubaliwa, zichukuliwe hatua kwani hiyo itakuwa fundisho kwa wale wote ambao wamekuwa wakihujumu miradi ya serikali na kusababisha wananchi kuendelea kuwa masikini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kushindwa uchaguzi vyama vya upinzani iwe fursa kujipanga upya

**UCHAGUZI** mkuu wa sita ndani ya mfumo wa vyama ulifanyika mwaka jana, huku vyama vya upinzani vikiendelea kushindwa, lakini safari hii vikiwa vimeshindwa kwa kishindo kana kwamba ni mara ya kwanza kushiriki uchaguzi huo.

Katika uchaguzi wa kwanza uliofanyika mwaka 1995, upinzani ulifurukuta na kufanikiwa kupata madiwani na wabunge wachache, huku kwenye nafasi ya urais vikibaki kusindikiza tu.

Tangu wakati huo vimeendelea kuishia kwenye nafasi hizo mbili, ambazo katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana vilijikuta vikiambulia majimbo mawili ya ubunge na madiwani wachache zaidi. Kwa hali ilivyo sasa, ni wazi kwamba kuna haja vyama hivyo kukaa na kutafakari ni wapi vimekosea na iwe ni fursa ya kujipanga upya, hasa baada ya kushindwa kwa kishindo katika uchaguzi huo wa mwaka jana.

Kutokana na hali hiyo, visichukulie matokeo hayo kwa hamaki bali iwe ni fursa ya kuviwezesha kujipanga upya ili virudi kwenye mstari na hatimaye viibuke na ushawishi kwa wananchi ili baada ya miaka mitano vije na mambo mapya.

Kutafakari na kujipanga upya kutavisaidia kujipanga upya ni njia mojawapo ya kuvifanya vionekane vinafanya kazi na kujitutumua katika maeneo mbalimbali nchini, hasa ngazi ya chini ambako ndiko kwenye wapigakura.

Visichoke kuwa na kazi ya ziada, hasa kuleta mvuto mzuri kwa staili mpya ya kuwafikia wapigakura ambao inawezekana wakakata tamaa kama vitaendelea kulalamika bila kuchukulia hatua ya kushindwa kama fursa ya kujipanga upya.

Njia mojawapo ya kuleta mvuto kama nilivyoeleza ni kujitanua zaidi kwenye maeneo ya chini, ambako kuna wanachama, ili viweze kuungwa mkono na watu wengi badala ya kujulikana juu tu kusikokuwa na wanachama.

Ikumbukwe kuwa vyama vya upinzani kutojitanua kwenye ngazi za chini, ili kuungwa mkono ni kosa ambalo limekuwapo kwa muda mrefu tangu kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi nchini. Hivyo ni muhimu vibadilike, na ikiwezekana, viige mfano kwa CCM ambayo ina mashina na matawi kote nchini, kwa kuwa huko ndiko waliko wanachama na wapigakura, na siyo mashabiki tu wasio na msimamo.

Sina maana kwamba upinzani hauna wanachama ngazi ya chini, lakini idadi yao ingeongezeka iwapo vyama hivyo vingekuwa na mkakati ya kujiimarisha ngazi ya chini kama ilivyo kwa CCM.

Mchango wa vyama ni muhimu kwa maendeleo ya taifa, lakini navyo viwe na mkakati wa kujiimarisha, kwa kufuata wanachama ngazi ya chini na kufungua ofisi za kutosha, ili kujihakikishia wingi wa wanachama.

Miaka 25 tangu uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi nchini ni mingi ambayo inatosha kuwafanya viongozi wa vyama hivyo kubuni mbinu mbalimbali za kuviwezesha kuendelea kuwa imara.

Lakini kikubwa zaidi kama nilivyoeleza awali, ushindi wa kushindo wa CCM, katika uchaguzi uliopita, uwe ni fursa kwa upinzani kujipanga upya badala ya kulalamika tu na kujikuta vikitoweka rasmi katika siasa za Tanzania.

Ni wakati wa vyama hivyo kujiuliza maswali mbalimbali ikiwamo wagombea wao waliungwa mkono na wapigakura hewa, ambao siku ya uchaguzi hawakujitokeza katika vituo vya kupigia kura? Si siri kwamba uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo huo uliofanyika mwaka 1995, ulikuwa na mchuano mkali na kusababisha vyama hivyo kupata madiwani na wabunge.

Tangu wakati huo, vimeendelea vizuri hali iliyoonyesha kuwa ni mwelekeo uliopanua mazingira ya kisiasa, ambayo yaliwapa watu uhuru zaidi na njia ambazo wangeweza kutolea maoni yao au kukosoa chochote kilichofanyika kinyume na masilahi yao.

Hata hivyo, migogoro ndani ya vyama hivyo ni moja ya matatizo yanayovikumba na kuvifanya viyumbe na kusababisha vikose nguvu na hivyo kutoaminika kwa wapigakura.

Kwa wanaofuatilia siasa za Tanzania, watakuwa wanajua kuwa wapo baadhi ya wanasiasa waliokimbia vyama vyao, kwa sababu ya migogoro isiyoisha, ingawa ni suala la kutofautiana katika taasisi ni jambo la kawaida.

Ni vyema kutafuta njia sahihi za kumaliza tofauti, ili zisisababishe migogoro, ambayo mwisho wake ni kuyumba kwa chama na kukifanya kisiwe na nguvu za kushawishi Watanzania.

## FIKRA MBADALA

# Tubadili sheria zetu haraka kuepuka lawama



Nkwazi Mhango, Canada

**Hivyo, watalifanyia kazi haraka kama ilivyokuwa utoroshaji madini kwa kuzungushia wigo machimbo ya tanzanite Mirerani na kuonyesha ufanisi wa hali ya juu.**

KATIKA kufunga mwaka 2020, vyombo vya habari viliripoti kisa funga mwaka ambapo Watanzania wawili walipatikana na hatia ya kujaribu kutorosha almasi zenye uzito wa karati 71,654 zenye thamani ya shilingi bilioni sita na ushee.

Vito hivi vya thamani vilitaifishwa baada ya mahakama kuwakuta na hatia watuhumiwa. Ajabu ya maajabu, badala ya kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi ili kupewa adhabu kali, wahusika waliamriwa kwenda jela miaka mitatu au kulipa faini ya shilingi milioni moja! Walilipa faini na kurejea kwenye uhalifu wao.

Mbali na kisa hiki, vyombo vya habari viliripoti kubanwa na kurejesha chumo la wizi kwa wezi wengine wakubwa baada ya kuingia makubaliano na mwendesha mashtaka wa serikali.

Kama nchi tunataka kutenda haki na kunufaika na mali zetu tulizopewa na Mungu, shurti tufute sheria zinazotoa nafuu na motisha kwa wahalifu. Lazima tuwe na sheria kali kushughulikia ujambazi huu ambao madhara yake ni makubwa kwa wananchi walio wengi. Kimsingi, sheria hizi zinazowapa motisha na nafuu wahalifu zilitungwa na wakoloni ili kujilinda. Kwanini aliyeiba kuku afungwe badala ya kurejesha kuku aliyemwiba? Bunge linapaswa kuliangalia hili kwa makini kama kweli wanawawakilisha Watanzania tena maskini.

Naamini Rais John Magufuli atasoma makala hii kama si yeye, basi washauri wake wenye mapenzi mema na nchi yetu. Hivyo, watalifanyia kazi haraka kama ilivyokuwa utoroshaji madini kwa kuzungushia wigo machimbo ya tanzanite Mirerani na kuonyesha ufanisi wa hali ya juu. Kama kweli kutorosha madini ya mabilioni kama haya adhabu yake ni kwenda jela miaka mitatu au kulipa faini, kwanini yeyote mwenye akili timamu asijaribu kamari hii inayolipa kirahisi na bila hatari kubwa yoyote?

Kama serikali haitakata rufani na kuwabadilishia mashtaka wahusika kwenda kwenye uhujumu uchumi, itajenga picha kuwa wahusika ni mawakala wa wakubwa wasiotaka wafungwe ili mwishowe wasimwage mtama kwenye kuku wengi. Hii inanikumbusha kesi moja maarufu iliyomhusisha mwizi mmoja toka India iliyohusisha wizi wa mabilioni ya fedha kwa kutumia mashamba yasiyoendelezwa ya mkonge.

Wizi huu ulipogundulika, wakubwa waliokuwa wakinufaika nao, walimfukuza nchini mhusika na taifa likapoteza mabilioni ya fedha.

Kama nilivyogusia hapo juu, nyingi ya sheria tunazotumia kwenye nchi za Kiafrika zilitungwa na wakoloni ili kurahisisha na kuwezesha ukoloni, unyonyaji na wizi kwao. Katika kufanikisha hili, wakoloni walianzisha makosa yanayojulikana kama white-collar crimes au jinai inayotendwa kwa kutumia kalamu.

Na kinachoendelea ni hiki ambapo wezi wengi wa kutumia kalamu ima hutozwa faini au kufungwa vifungo vifupi. Jinai hii, mara nyingi, hutendwa na watumishi wa umma, watawala, matapeli, wafanyabiashara na wengine wa kada hizi. Katika kuhalalisha jinai hii ya kimfumo, ukoloni ulikuja na msemo usemao kuwa the pen is mightier than a sword; yaani kalamu ni bora kuliko upanga. Hata madhara yatokanayo na kalamu kiuchumi ni makubwa kwa nchi na watu wake kuliko ya upanga. Mfano, fedha zinazoibiwa na majambazi kwa kutumia silaha ni kidogo kulinganisha na zinazoibiwa kwa kalamu.

Na kutokana na kuacha sheria hizi bila kurekebishwa, wapo wanaosoma siyo kutumikia wala kusaidia taifa bali kutumia kalamu au elimu kulihujumu kama ambavyo Afrika imeshuhudia tangu kupata uhuru wa bendera ambao haukuleta nafuu kwa watu wetu.

Katika mambo ambayo safu hii imekuwa ikipigia kelele ni mfumo mzima wa uendeshaji nchi zetu za kiafrika. Mfano, katika nchi zilizotutawala, huwezi ukaishi bila kuelewa kipato chako ni kiasi gani na kinatokana na nini. Lakini kwa upande wa Afrika, mtu analala maskini anaamka tajiri.

Mamlaka hazimhoji au kumkamata na kumtaka aeleze alivyopata utajiri wake! Hapa Kanada, ikitokea, majirani wataripoti kwa serikali ambayo itakukamata wewe na mali zako hadi utakapotoa maelezo yanayoingia akilini. Kwa namna hii, hapa wizi hauna tija wala hakuna motisha kwa watu kuibia wenzao au serikali. Wanaogopa watakamatwa. Je hali ikoje kwetu?

Wapo watu tunaowajua kwa sura na majina waliotajirika kwa kuibia nchi. Badala ya kuwakamata tunawanyenyekea na kuwaendekeza.

Leo sitaongelea hili sana. Nitalidurusu kwenye makala zijazo nitakapotoa ushauri wa nini kifanyike kwa wafanyakazi na waliokuwa wafanyakazi wa baadhi ya idara za serikali ambao walitumia fursa zao kuliibia taifa wakastaafu na kuendelea kutumbua ukwasi wa wizi.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Hivi ndugu ilitukosea nini waheshimiwa!



Na Joseph Kulangwa

**Maria Nyerere, Mama Sophia Kawawa, na kadhalika. Kumbe wenye akili wakawa wanawaza na kuwazua, kuhusu utambulisho huu. Wakauona kama una chembechembe za kikoloni bado. Wakaona kumbe zina chembechembe za kibaguzi pia.**

ENZI za mwishoni mwa ukoloni Tanganyika, tuliokuwa tunasikia na kuelewa na hata tukisikiliza redio za Rising na Phillips, tulizoea kumsikia Mwalimu Julius Nyerere akiita au kuwatambulisha Bwana Edward Twinning au Bwana Richard Turnbull.

Hao walikuwa ni magavana wa mwisho mwisho wa Mkoloni Mwingereza nchini. Lakini hata Nyerere alitambulishwa kama Bwana Julius Nyerere na wenzake au wadogo zake kiwadhifa, alipokuwa mikutanoni na kokote alikotakiwa kutambulishwa.

Nyakati hizo hata wanawake walitambulishwa, kama vile Bibi Titi Mohammed, Bibi Maria Nyerere, Bibi Sophia Kawawa na wanawake wengine maarufu walitambulishwa hivyo tukiona wazee wetu wakikubaliana kabisa na utambulisho huo wa Bwana Fulani au Bibi Fulani.

Baadaye tukaambiwa Bwana ni utambulisho wa mmiliki wa mtumwa, hivyo mtumwa alimwita mmiliki wake Bwana wangu. Kwa kuwa mfumo ulikuwa ni dume, tulisikia Bwana zaidi ya Bibi, huku bibi akibaki kuwa mke wa bwana. Ingawa kwingineko, bibi alikuwa nyanya. Mama wa baba au mama yako.

Kidogokidogo, bibi fulani ikafa, ikabaki mama fulani. Tukaanza kusikia Mama Maria Nyerere, Mama Sophia Kawawa, na kadhalika. Kumbe wenye akili wakawa wanawaza na kuwazua, kuhusu utambulisho huu. Wakauona kama una chembechembe za kikoloni bado. Wakaona kumbe zina chembechembe za kibaguzi pia.

Wenye akili hao, wakaona kuwa kumbe kuitana bwana fulani, kunamaanisha kuwapo utumwa miongoni mwa Watanganyika. Hata baada ya Uhuru mambo yaliendelea hivyo hivyo, bwana na bibi fulani, kabla ya bibi kuwa mama fulani.

Ilipobainika zaidi kwamba kumbe utambulisho huu ututugawa, ikaonekana bora tuitane waheshimiwa. Yaani kiongozi aitwe mheshimiwa fulani bila sasa kujali ni bwana au bibi. Mheshimiwa Julius Nyerere, Mheshimiwa Rashidi Kawawa, Mheshimiwa ikawa mheshimiwa kila mahali. Majaji na mahakimu wakawa waheshimiwa.

Wabunge na madiwani nao wakataka wawe waheshimiwa, kwa kuwa wanatunga sheria za nchi na maeneo, michakato ikafanyika, wakawa waheshimiwa. Mwananchi wa kawaida akabaki mwananchi wa kawaida. Aitwe mheshimiwa kivipi wakati hana cheo wala wadhifa!

Hiyo nayo ikaonekana inaleta utengamano badala ya utangamano. Wenye vichwa vyao wakakaa na kutafakari, wakaona umoja wetu ulioleta uhuru kwa kuunganishwa na Kiswahili, utaparaganyika kama nchi itakuwa ya waheshimiwa na wasioheshimiwa, wakati Katiba inasema kila mtu ana haki ya kuheshimiwa na hivyo ni mheshimiwa, kwa nini sasa wawe wachache nchini. Tunagawanyika ohoo! Mwalimu Nyerere akaliona hilo, akashauriana na wenzake, wakajiuliza kwa nini tusiitane ndugu? Mbona hilo halina ubaguzi, kwa kuwa sisi ni ndugu na tunaapa kuwa Afrika ni moja na kila mtu ni ndugu yangu! Ikakubalika tuitane ndugu, bila kujali umri, kabila, dini au rangi ya mtu.

Ndugu ikatuunganisha, ikatuheshimisha na kututambulisha kimataifa. Rais wa Tanzania, Ndugu Julius Nyerere, Waziri Mkuu, Ndugu Rashid Kawawa. Ikawa hivyo, mpaka majirani zetu nao tukaanza kuwaita ndugu. Rais wa Kenya, Ndugu Jomo Kenyatta, Rais wa Uganda, Ndugu Milton Obotte.

Kwa kweli Nyerere akaipenda sana, akiitumia sana kila alikohitaji kutambulisha au kuhutubia, isipokuwa kwa viongozi wa dini, Baba Askofu au Shekhe Mkuu. Huko hakutumia ndugu hata kidogo. Alikuwa mnyenyekevu kuliko kawaida.

Ilibaki kidogo tu ndugu iwe utambulisho wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa sababu ilionekana inatuunganisha na kutuheshimisha. Iliishia wapi? Mungu mwenyewe anajua, kwa kuwa tulikuwa na Kiswahili wenzetu wakiwa na makabila.

Mara he, ndugu ikajifia tena, tukasikia wabunge wanataka waitwe waheshimiwa, kama majaji, mahakimu, na madiwani nao wakafuata nyayo. Ikaja kwa maarasii, madisii, madedi, madasi, wenyeviti wa mitaa, mabalozi wa nyumba 10, wakachekelea.

Polepole uheshimiwa huu unaanza kutugawa, wale kule, hawa huku. Wa juu wa juu, wa chini wa chini! Waheshimiwa wanacharaza ndugu bakora hadharani. Wanajua kabisa sheria zinasemaje kwa mkosaji. Wanajua kabisa mahakama zimejengwa kwa minajili gani, lakini wanacharaza tu. Sisi ni ndugu, tujiulize tunakokosea, turudi tuitane ndugu, nyadhifa au vyeo haviondoki kwa kuitana ndugu, ila tunashikamana zaidi. **Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Viongozi kuwacharaza watu viboko kulianza tangu wakati wa Nyerere



Na Thobias Mwanakatwe

NI Januari 2, 2021 saa 3:00 usiku, nikiwa nyumbani kwangu nikifuatilia kipindi cha Papo kwa Papo kinachorushwa na luninga ya Channel Ten, nikamsikia mwananchi mmoja akipiga simu na kulalamika mfululizo wa matukio ya viongozi wa umma kuwacharaza bakora wananchi.

Mwananchi huyo kutoka Mtwara alisema kitendo kinachofanywa na viongozi wa umma ni cha udhalilishaji na kushangaa ni kwa nini viongozi wa juu wa serikali hawajakemea jambo hili ambalo linazidi kuota mizizi.

Ukilitazama jambo hili malalamiko ya mwananchi huyu ni kama amewakilisha mamia na maelfu ya wananchi wa Tanzania ambao kwa mtazamo wao vitendo vinavyofanywa na viongozi wa umma kuwacharaza bakora watu wanaotuhumiwa kwa makosa mbalimbali ni uvunjifu wa sheria.

Malalamiko hayo ya wananchi kwa mara ya kwanza yalianza kuhojiwa Oktoba 4, 2019 baada ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kuwacharaza viboko na kuwaondoa shuleni wanafunzi wa kidato cha tano na sita katika Shule ya Sekondari Kiwanja, wilayani Chunya kwa madai ya kuchoma moto mabweni.

Wakati tukio hilo halijapoa, naye Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenani Kihongosi, akawacharaza viboko wanafunzi watatu wa kidato cha kwanza wa Shule ya Sekondari Sinoni pamoja na wananchi wengine kwa tuhuma za kuiba viti 108 vya shule hiyo.

Suala la viongozi wa umma kuwacharaza viboko wananchi limekoleza zaidi malalamiko ya wananchi baada ya hivi majuzi, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Watu Wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga, kuwacharaza viboko watu waliodaiwa kudhalilisha walemavu jijini Dar es Salaam kwa kuwatembeza mitaani kuombaomba.

Kutokana na mfululizo wa matukio haya, nimeona niwakumbushe wananchi wafahamu kwamba vitendo vya watu kucharazwa bakora havijaanza leo bali vilikuwapo tangu enzi za utawala wa kikoloni na utawala wa Rais wa Awamu ya Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere.

Wananchi lazima wafahamu kwamba Tanzania tumerithi sheria za kikoloni ambapo kuna makosa ya jinai na makosa yasiyo ya jinai.

Nawakumbusha historia, Oktoba 21, 1966 uongozi wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam uliitisha kikao cha dharura na kuazimia kuandamana bila kibali cha polisi kwenda Ikulu kukabiliana uso kwa uso na Mwalimu Nyerere.

Waandamanaji waliandaa mabango yenye ujumbe mbalimbali, kwa kutaja baadhi tu, yalisomeka :"TUMECHOKA KUTUMIKIA WABENZI (mafisadi), "AFADHALI WAKATI WA UKOLONI", "KUMBUKA YA INDONESIA", "ATOKOMEZWE KAWAWA NA MPANGO WAKE WA JKT" na mengine mengi.

Maandamano hayo hayakuwahusisha vijana wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pekee bali walijiunga wengine wengi kutoka Chuo cha Uganga cha Muhimbili, Chuo cha Ualimu Chang'ombe, Chuo cha Biashara (CBE), Shule ya Sekondari Agha Khan na vijana 'wapita njia'.

Ikulu waandamanaji hao walilakiwa na Mwalimu mwenyewe, Makamu wa Pili wa Rais, Rashidi Mfaume Kawawa, na mawaziri. Mwalimu alimkaribisha msemaji mkuu wa waandamanaji kuelezea malalamiko yao naye bila kusita kwa lugha ya Kiingereza fasaha akatamka masharti yao kwa sauti ya ukali akisema;

"Serikali inajaribu kutupa mzigo wa kugharamia mpango huu (JKT) mabegani mwa wanafunzi maskini, ama tulipwe haki zetu zote za mishahara au wale wote wanaopata mishahara ya juu nao watumbukizwe katika utaratibu huu uonekane kweli ni wa kujitolea na si mpango wa kunyonya wasomi vijana pekee."

Akaendelea: "Kwa hiyo mheshimiwa kama utaratibu huu pamoja na mawazo ya viongozi wa juu hayakubadilika, hatukubali mpango wa JKT kwa moyo. Miili yetu inaweza kwenda lakini mioyo yetu itabaki nje ya mpango huu."

Alitamka kwa kujiamini na kwa kushangiliwa. Mwalimu alianza kujibu risala hiyo, pamoja na mambo mengine alisema; kwanza kwa upole na kwa sauti tulivu, akasema:

"Sasa mimi nimeyakubali masharti yenu, naweza kuwahakikishia kwamba sitamlazimisha mtu yeyote. Mnayosema ni sawa kwamba hata miili yenu ikienda JKT, mioyo yenu haitakuwa huko. Sitampeleka hata mmoja wenu JKT ambaye moyo wake haupendi (makofi) maana huko si gerezani. Mwisho alirejea kwenye hoja ya siku hiyo, akasema: "Mimi nimeyakubali maneno yenu mnayosema na ninyi nawaomba mwende nyumbani kwenu. Rashidi (yaani Kawawa) ni jukumu lako kuhakikisha kwamba wanakwenda kwao."

Alikuwa amewafukuza wanafunzi wote 415 mara wakazingirwa na Polisi, wakaanza kushughulikiwa na FFU kwa ulinzi na kudhibitiwa.

Hata hivyo, wanafunzi hao walirejeshwa mwaka 1969 pamoja na adhabu ya kuchapwa viboko kwa mkono wa Mwalimu mwenyewe. Kwa hiyo suala la viongozi wa umma kuwacharaza viboko watu halijaanza awamu hii ya serikali ya awamu ya tano.

**Kwa maoni na ushauri tuwasiliane katika barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com au WhatsApp 0762-183666**

## DARASA LA NDOA

# Tambua maadui wa ndoa yako - 2



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

NDOA ni taasisi kongwe kuliko zote tangu kuumbwa kwa ulimwengu. Ukongwe huo hauifanyi iwe katika hali shwari kila uchao kwani kama zilizo taasisi zingine, ndoa ina maadui mbalimbali ambao wanaweza kuishambulia na hata kusambaratika.

Sehemu ya kwanza ya mada hii, tulijadili maadui watatu ambao ni utoto katika ndoa, kauli mbaya na wazazi. Katika maadui hao, tuliona kila mmoja anavyoweza kusababisha ndoa kuyumba na wakati mwingine kuvunjika.

Katika mwendelezo wa mada hii, leo tutaangalia maadui wengine katika maisha ya ndoa ambao wanandoa wanapaswa kuwa makini nao. Maadui hao ni kama wafuatao;-

**MARAFIKI NA JAMAA**

Hatari nyingine inayozikabili ndoa nyingi ni kundi la marafiki na jamaa zetu. Marafiki wengi si waaminifu; si wajengaji wa familia za rafiki na jamaa zao. Mtu anaweza kuwa na marafiki lakini si kila rafiki anaweza kuwa mwema kwake. Mtu anaweza kuwa na ndugu, lakini si kila ndugu anamwazia mema.

Marafiki wengine wametumia mapungufu katika ndoa za rafiki zao kwa kujenga uhusiano mpya na wake au waume za rafiki zao. Waswahili wanasema kikulacho kinguoni mwako. Wengine wamefikia uamuzi wa kuvunja ndoa zao kutokana na ushauri wa marafiki (mashoga) ambao wengine hata hawajawahi kufikiri kuolewa au kuoa katika maisha yao.

Wengine wanashauriwa na watu waliokata tamaa na ambao maisha ya ndoa yamewashinda. Wengine waliolewa au kuoa lakini maisha ya ndoa yamewapiga. Mtu asitegemee neno jema kuhusu ndoa kutoka kwa mtu aliyeshindwa ndoa. Kwa vyovyote vile, atakuwa na uzoefu mbaya kuhusu ndoa. Uzoefu alio nao ni wa kushindwa na si kufanikiwa katika ndoa.

Aidha, wako baadhi ya wanawake wanaotamani sana maisha ya ndoa, lakini wanapoona siku zinaenda bila kupata mwenzi, wanafanya kila wawezalo kuleta fitina katika ndoa za wenzao ili mume amfukuze mkewe na yeye achukue nafasi.

Mfano, kuna bwana mmoja alimfukuza mke wake kwa sababu ya marafiki. Siku moja, mmoja wa rafiki za mke wake alimpigia simu huyu bwana akidai ana shida kubwa nyumbani kwake. Yule bwana akaenda na hakuwa na shaka naye. Lakini alipofika alishangazwa sana baada ya kuonyeshwa picha za video zikimwonyesha mke wake akiwa kwa mganga wa kienyeji alikokwenda kutafuta dawa ili amuue.

Huyu bwana alikasirika sana kwa kupata taarifa hizi. Aliporudi nyumbani kwake, bila kuuliza wala mazungumzo yoyote na mkewe, kwa hasira alimtimua mke wake usiku ule ule. Kesho yake akaja yule dada (rafiki wa mke wake) aliyempa taarifa ile. Yule dada akamwambia huyu bwana, yuko tayari kumfariji, akimaanisha kuchukua nafasi ya mke wake.

Hata hivyo, baada ya kuchunguza, aligundua alichoambiwa ulikuwa uongo uliokusudiwa kuvuruga ndoa yake. Alibaini kuwa taarifa aliyopewa kuhusu mkewe ilikuwa habari ya kupikwa. Yule bwana aliumia sana moyoni. Ni muhimu kufahamu kuwa wako marafiki wazuri ambao wamesaidia kuimarika kwa ndoa za wenzao. Lakini wako marafiki wabaya ambao kazi yao ni kuharibu ndoa za wenzao kama tulivyoona katika mfano hapo juu.

Mfano mwingine, yuko mwanamke mmoja aliamua kuondoka kwa mumewe kwa sababu alipata taarifa kwamba kila anapoondoka kwenda kazini, muwewe analeta wanawake wengine nyumbani. Mwanamke huyo bila kuchunguza, alianza kufanya ukahaba tena kwa kusaidiwa na kushawishiwa na wale wale waliokuwa wakimletea taarifa za mumewe, akidai analipiza kisasi. Ndoa hiyo haikudumu. Ilivunjika!

**KAZI NA KIPATO**

Baadhi ya waajiri na viongozi wamechangia sana kuvurugika kwa ndoa za watumishi walio chini yao. Mahali pengine baadhi ya wakuu wamelazimisha mahusiano ya kimapenzi na watumisi walio chini yao.

Wengine hudiriki kutoa ofa za upendeleo kama vile safari, kazi za muda wa ziada na kuwa mstari wa mbele kutatua matatizo yanayomtokea mfanyakazi wake. Uhusiano huo mapya, umesababisha baadhi ya watumishi kudharau, kutokujali na kutokuthamini waume au wake zao nyumbani. Hali hii huleta migogoro isiyoisha.

Matatizo mengine katika ndoa yametokana na kipato ndani ya familia. Wako wanandoa waliovuruga ndoa zao kutokana na tamaa tu ya kutaka maisha ya juu yasiyolingana na uwezo wao. Wengine tafauti yao ya vipato na nafasi zao kikazi, vimekuwa sababu ya ugomvi katika ndoa kwa sababu ya kukosa kuheshimiana.

**UASI KWA MUNGU**

Ndoa nyingi zimeanguka kwa sababu ya kukosa hofu ya Mungu. Matatizo yalianza hata kabla ya ndoa yenyewe kufungwa. Sababu kuu ni kuanza na kuendelea na maisha ya ndoa bila Mungu. Uthibitisho wa hili ni dhahiri kwani maandalizi ya harusi nyingi yamejikita katika mambo ya kimwili zaidi kama kuvaa, kula, kunywa na kusherehekea. Mungu hapewi nafasi katika maandalizi ya harusi zilizo nyingi.

Ni nadra kusikia kuwa, kuna kamati ya maombi ya harusi. Aidha, hata wanaoshiriki ibada ya ndoa katika nyumba za ibada idadi yao huwa ni ndogo sana, ikilinganishwa na wanaoshiriki sherehe ukumbini. Wengine hata sadaka ya shukrani kwa Mungu kwa ajili ya kufunga ndoa hawatoi na hawajiandai. Hata wakitoa, matoleo yao hayaakisi gharama halisi iliyotumika kuandaa harusi. Watu wanaishi na kuenenda kana kwamba wamejileta wenyewe duniani.

Ni muhimu ifahamike kuwa furaha na amani katika ndoa, haviletwi na fedha, mali, elimu kubwa, cheo na kazi nzuri au gari zuri bali Mungu pekee ndiye wa kuzifanya ndoa zetu kuwa nzuri na salama, tukimtanguliza na kumtegemea.

Fedha, elimu, mali, nafasi zetu za kazi visipofungamanishwa na Mungu, huwafanya watu kuishi maisha yaliyojaa mihemko na yasiyo na furaha halisi. Hivyo, uhusiano wetu na Mungu, lazima utangulie mahusiano yetu ya ndoa. Kumbuka, hakuna baraka nje ya Mungu. Nje ya Mungu ni mikosi, laana na kushindwa.

Nawatakia wanandoa wote mwaka mpya 2021 wenye heri, amani, utulivu na umakini!

■ **Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maoni, mafunzo na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au WhatsApp +255655865555.]**

# MAISHA

Januari 10, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




## NI HARUSI YA KALONGA KASATI NA NURU MWAISANGO

iliyofungwa Kanisa la T.A.G Majumba Sita, Desemba 5, 2020 na kufuatiwa na tafrija iliyofanyika Kebby`s Hotel, Mwenge, jijini Dar es Salaam.

## HARUSI

Ukurasa 12



Ukurasa 15


## MAISHA NI NYUMBA

Usafi wa kitanda ni muhimu nyumbani

## Matoke ya mboga

Ukurasa 14





## JICHO NI KILA KITU

# Urembo unaosema wenyewe

Ukurasa 14

# Sio uchawi ni tatizo la kisaikolojia

Na Moses Ismail

VIJIJINI wazazi wengi hutafuta sababu za chanzo cha kutoelewana na watoto wao kupitia kwa waganga wa kienyeji. Wanachoamini wao ni lazima kutakuwa na mkono wa mtu. Iweje wao na watoto wao wasielewane?

Wanafanya hivyo pale wanapoona watoto wao wakubwa, wenye uwezo wa mali na fedha, wanashindwa kuwasaidia hata kwa mambo yao madogo tu yanayohitaji fedha. Wanaamini hilo haliwezi kutokea bila ya 'mkono wa mtu'.

Hilo limewahi kutokea baina ya bibi Edith Mgaya, mama mkazi wa Chamazi, nje ya jijini Dar es Salaam. Yeye na mwanawe hawakuwa wakielewana kabisa.

Bibi Mgaya anasema: "Ilifikia mahali mwanangu alikuwa hakanyagi nyumbani hata miezi minne mpaka mitano, namuona tu anapita barabarani na gari yake."

Hali hiyo ikamfanya bibi Mgaya kuamini kuwa si bure, lazima kuna mkono wa mtu kwa sababu mtoto wake alikuwa na uwezo mkubwa wa mali, akaenda kwa mganga.

"Mwanangu wachawi wapo." Anasema bibi Mgaya na kuongeza: "Kumbe alikuwa amelogwa. Alitupiwa kitu ili kila tukizungumza tusielewane. Basi mganga akanipa dawa. Akaniambia nimuite mwanangu niongee naye vizuri na nile naye chakula bila ya kupishana naye maneno. Hivi ninavyozungumza na wewe miaka sita sasa tunaelewana."

Ni kweli, kwa imani za kiroho vitabu vitakatifu vinautaja uchawi, vinaeleza athari ya kitu hicho na vinakataza kuutumia kwa vile ni kitu kibaya chenye madahara kwa watu, lakini, katika hili la mzazi na mtoto 'kuwa mbalimbali' ni uchawi ndio unaosababisha?

"Jibu haliwezi kuwa la moja kwa moja", anasema Denis Munga, mtaalamu wa masuala ya saikolojia na kufafanua:"Haliwezi kuwa la moja kwa moja kwa sababu pamoja na kwamba uchawi upo na watu wanauamini, lakini katika kesi nyingi za mzazi na mtoto kutoelewana suala la saikolojia linachukua nafasi kubwa sana".

Munga anafafanua zaidi kwa kutumia mfano: "Mfano wazazi wenye tabia ya kupenda kutokaa pamoja na watoto wao, hawa wanajenga tatizo hilo wenyewe, kutopenda kuwa karibu na mtoto wako wakati akiwa mdogo kunajenga ufa baina yenu.

"Ufa huu ukiendelea kwa muda mrefu, yanakuwa ni maisha ya kawaida baina ya mzazi na mtoto, hata kama mtoto atakuwa na umri wa miaka hamsini, kwa sababu msingi ulishajengwa tangu utotoni".

Kwa ufafanuzi huo, Munga anakataa kuchukulia suala la uchawi kama sababu pekee ya jambo hilo na anashauri wazazi kutafuta majibu ya tatizo hilo kwa wataalamu wa saikolojia zaidi ya kutafuta sababu za gizani.

Kuzungumza na mtoto wako na kumshirikisha katika masuala ya kifamilia tangu akiwa mdogo ni jambo muhimu sana, kumtenga na kumfanya asiwe na thamani au kupenda kumfokea kila mara ndiyo sababu kubwa inayomfanya ajitenge nawe.

Wazazi wengi wanaoshindwa kushirikiana na watoto wao katika hali ya utu uzima wanavuna matunda ya ukali waliuonyesha kwa watoto wao walipokuwa wadogo.

## QUIZ

NA HAMIS KIDAGO
0657 207168

Le quiz du week

***Comment t'appelles – tu?: Unaitwa nani?***

1. Soma dayolojia ifuatayo katika lugha ya Kifaransa na ujaze sehemu zilizokuwa wazi.


**Dayolojia**

*Katika lango kuu la kuingia katika Shule ya Sekondari, baada ya likizo ya masomo kuisha, Raswiina na Sarah wanakutana na marafiki wapya.*

**Raswiina:** Salut!
**Sarah:** Salut!
**Raswiina:** Comment vas – tu?
**Sarah:** Je vais bien, merci. Et toi?
**Raswiina:** Je vais bien egalement.
**Sarah:** Comment t'appelles – tu?
**Raswiina:** Je m'appelle Raswiina.
**Sarah:** Moi, c'est Sarah. Je suis de Dodoma.
**Raswiina:** Je suis ravi de te connaitre, Sarah.
**Sarah:** Moi de meme.
**Sarah:** Quel est le nom de ta copine?
**Raswiina:** Elle s'appelle Mariam. Elle vient de Kilimandjaro comme moi!
**Sarah:** Salut Mariam, je suis contente de faire ta connaissance!
**Mariam:** Je suis contente egalement de te connaitre, tu es sympathique!
*Sarah anamuita rafiki yake mmoja wa darasani ambaye anakuja akikimbia.*
**Sarah:** Je vous presente ma meilleure amie. Elle s'appelle Nathalie. Elle est francaise d'origine espagnole. Elle est en Tanzanie pour une annee. Elle habite dans ma famille. On est dans la meme classe.


## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA KIDOGO

Mazungumzo kati ya marafiki wawili yalikua kama ifuatavyo;
JAMAA: Habari yako kijana?
RAFIKI: Safi tu nambie,
JAMAA: Aiseee! muda mrefu kweli naona unaangaika na bodaboda tatizo nini?,
RAFIKI: Dah! Namsaidia huyu mwanamuziki kupata kiki ili aonekane haraka.
JAMAA: Ooohhhh!! Kweli mzima!



SWALI
Taja faida ya mnazi

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Wazazi wa mchumba wanapomkataa kijana kisa anatoka familia maskini

KARIBU tena msomaji wangu katika makala yetu ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo nikupe simulizi ya kijana aliyekataliwa na wazazi wa mchumba, kisa anatoka familia maskini. Ni kijana aliyefikisha umri wa kuoa, akampata mke mtarajiwa, lakini akamponyoka dakika za mwisho. Nini kilitokea?

Kijana huyu alijikuta anakataliwa na wazazi wa mchumba wake eti kwa sababu anatoka familia maskini na pia elimu yake ilikuwa ni ndogo. Alikuwa anajishughulisha na biashara ndogo ndogo za kuuza vifaa vya simu, 'umachinga'.

Akiwa katika harakati za kutafuta fedha kupitia biashara zake, alifanikiwa kukutana na dada mmoja, jina Josepha aliyekuwa akisoma shahada ya sheria katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine. Wakapendana sana na kuahidiana kuoana.

Siku moja akiwa likizo, yule binti alimwomba mchumba wake aende kujitambulisha kwao Ruvuma ili familia yake wamjue. Yule kaka aliheshimu mawazo ya mchumba na kuchukua uamuzi kwenda kujitambulisha.

Alipofika wazazi wa yule binti walimkaribisha na kuanza kumhoji maswali. Ukweli ni kwamba alikuwa na sifa zote za nje za kuoa kutokana na utanashati wake, heshima yake aliyokuwa nayo, ustaarabu na usafi wa mwili, isipokuwa elimu yake ilikuwa kidato cha nne.

Ilipofika kwenye suala la elimu, aliwaeleza kuwa hakuweza kuendelea na elimu ya juu kwa kukosa ada kutokana na wazazi wake wote kufariki dunia na hakuwa na uwezo wa kujiendeleza tena isipokuwa kutafuta fedha kwa ajili ya kuendeleza maisha yake.

Kitu cha kushangaza, wale wazazi wa binti waliinuka ghafla na kuanza kusema: "Binti yetu hawezi kuolewa na mwanaume ambaye hajasoma. Tumetumia fedha nyingi kumsomesha mtoto wetu ili awe na maisha mazuri, si kuja kuolewa na mtu baki.

"Ni kweli una sifa zote za kumuoa binti yetu, lakini kwa sababu hujasoma, tunaomba umwache binti na tusisikie umemkaribia kwa namna yoyote ile, kwa maana tukisikia tutakufunga (kushtaki)," walimaliza kusema.

Kijana yule alihisi baridi ghafla. Alihisi uchungu usio wa kawaida na kuondoka pale akisema kwa machozi; "nanyimwa mke, kisa sijasoma? Iko siku na mimi Mungu atanisaidia tu. Kumpenda binti yenu sio sababu ya kushambulia elimu yangu ndogo kwani nilitamani kufika mbali. Nilifaulu kidato cha nne lakini hakupatikana mtu wa kunisomesha. Wazazi wangu walikufa"!

Haikuwa rahisi kwake hata kidogo kutokana na kwamba alitumia gharama zake za kusafiri kwenda Ruvuma, badala ya kukubaliwa walimkataa, tena kwa jambo ambalo hakuwa na uwezo nalo wakati ule. Aliumia sana. Lakini kupitia maumivu yale, akajikuta akipata nguvu ya kuendelea na masomo.

Mpenzi msomaji, baada ya hapo alichofanya kijana alianza kutunza kila faida ya biashara yake kwa ajili ya ada. Ilipotimia kiasi fulani alijisajili kwenye Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (QT). Akamaliza kidato cha sita na kujiunga kwenyeC cha Mtakatifu Augustine kwa ajili ya kuchukua shahada ya mambo ya uchumi na biashara.

Baada ya miaka mitatu ya chuo alihitimu na wakati huo alikuwa tayari amefungua duka kubwa la simu mjini Mwanza. Akawa anafuata bidhaa Dubai na China.

Miezi kadhaa baada ya kuhitimu chuo, alikutana na binti mmoja wa Kitanzania nchini China, akiwa katika harakati za ununuzi wa mzigo wa biashara. Wakapendana na huyo binti ambaye alikuwa amehitimu shahada ya utabibu nchini humo.

Waliporudi nchini wakafunga ndoa na sasa wana watoto watatu wanaishi Dar. Cha kushangaza, yule binti ambaye wazazi walikataa asiolewe alikuja kuzalia nyumbani na hadi sasa yuko kwa wazazi wake.

Msomaji wangu, binafsi nimejifunza kutodharau mtu yoyote hata kama ana hali ngumu kiasi gani. Pia tujue chochote kinachotokea kwenye maisha yetu, kina kusudi, iwe ni kizuri au kibaya. Naamini kuwa kaka huyu kama asingekutana na upinzani, asingekuwa na uchungu kujiendeleza. Kukataliwa kuliamsha kitu ndani yake na kukubali kurudi shule.

Unapokataliwa usivunjike moyo. Badala ya kulaani, jifute machozi, jitie moyo, songa mbele. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Tuishie hapa. Je, una maoni, ushauri au kisa cha kimaisha? Nitumie ujumbe kupitia 0715268581. Namba hii pia ipo WhatsAAP.

**Msomaji wangu, Lazima watu watafute sana nguvu ya Mungu kufuta hayo maneno. Mungu ni mwaminifu, huchunguza mioyo, tukiomba kwa dhati laana za aina hiyo hufutika.**

**Tuishie hapa hadi wiki ijayo. Ukiwa na kisa, maoni, ushauri nitumie ujumbe kupitia 0715268581. Namba hii pia ipo WhatsAPP.**

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Hatua zichukuliwe kuinusuru Mamlaka Hifadhi Ngorongoro

MAMLAKA ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), imepaza sauti juu ya tishio la uhai wa eneo hilo muhimu kwa uhifadhi ambalo ni urithi wa dunia.

Wakati hifadhi hiyo inaanzishwa mwaka 1959 ilikuwa na watu 4,000 na baadaye waliokuwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti walihamishiwa ndani ya Ngorongoro ili kupisha uhifadhi wa asilimia 100 ndani ya eneo hilo na kufanya watu kuwa 8,000, awali lilijulikana kama Serengeti Game Reserve.

Eneo la Ngorongoro ni pekee duniani kwa kuwa binadamu na wanyama wanaishi pamoja, na hali hiyo imevuta idadi kubwa ya watalii kiasi cha kufikisha magari zaidi ya 1,000 ndani ya Creter kwa siku moja.

Kwa sasa hali ni tofauti kabisa kwa kuwa idadi ya watu imeongezeka na kwa mujibu wa sensa kuna zaidi ya watu 100,000 na malaki ya mifugo ambayo inaongezeka siku hadi siku.

Mbaya zaidi, mifugo hiyo inamilikiwa na asilimia 20 ya watu huku asilimia 80 hawana mifugo na licha ya jitihada mbalimbali za kujenga huduma za jamii kama shule na hospitali, kiwango cha kutokujua kusoma na kuandika ni zaidi ya asilimia 64.5.

Kwa sasa NCAA wanasema kila jitihada ya uhifadhi inayofanyika inakuwa na madhara ya moja kwa moja kwa jamii husika, na kila ongezeko la mifugo na binadamu ndani ya hifadhi lina madhara kwa utalii na uhifadhi.

Nilipata bahati ya kutembelea eneo hilo na kujionea makundi ya ng'ombe, mbuzi na kondoo ambao wanachungwa na kula pamoja na wanyamapori.

Kama haitoshi, binadamu anaishi kwa mabadiliko mbalimbali ikiwamo kubadili muundo wa maisha yake, na ndani ya hifadhi hiyo watu wanaoishi humo walitakiwa kuishi kwa uasili wao pasipo kujenga nyumba za kisasa waka shughuli za kilimo.

Lakini kutokana na mabadiliko ya maisha wanaondokana na nyumba za nyasi ambazo ni za asili yao na kuwa na nyumba za kisasa za bati, huku wengine wakiacha kutegemea nyama na maziwa kama chakula na kutaka kula vyakula kama ugali na vinginevyo.

Moja ya jitihada zilizofanywa na NCAA ni kutoa ufadhili wa masomo kwa wananchi wa eneo hilo, lakini bado kiwango cha ujinga kiko juu jambo ambali linahitaji kuchukua hatua za haraka kusaidia jamii hiyo.

NCAA inaeleza wazi kuwa hali ikiachwa ilivyo miaka 10 ijayo uhifadhi utakuwa katika hali ngumu sana, ni muhimu sana hatua zikachukuliwa na hakuna ubishi kuwa ni lazima binadamu waliopo ndani ya eneo hilo wakapunguzwa, idadi ya mifugo na shughuli za kijamii.

Hakuna ubishi kuwa sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza eneo hilo zinapaswa kupitiwa upya ili kuon akama bado eneo hilo linaweza kuendelea na changamoto hizo au nini kifanyike ili uhifadhi uendelee na binadamu wawepo kwa kuwa watalii wanakuja kwa kuwa wanataka kujifunza mwingiliano wa maisha baina ya binadamu na wanyamapori.

Miaka ya nyuma hatua zilichukuliwa kwa kuhamisha kaya 119 kwenda eneo la Jema kutoka Oldonyosambu, na hilo lilisaidia kupunguza uharibifu na migogoro lakini kwa hali ilivyosasa ni lazima mabadiliko ya lazima ili kuounguza idadi ya watu na mifugo.

Kwa sasa kuna migogoro mikubwa baina ya binadamu na wanyamapori kwa kuwa sasa Simba na wanyama wengine wanavamia maboma wanakula mifugo na kuleta madhara kwa binadamu, na kunakuwa na vinyongo ambavyo hupelekea kulipiza kisasi kwa kuweka simu kwenye mizoga.

Mathalani, hivi karibuni fisi aliingia kwenye boma na kuua kondoo 30. Kwa hali ya kawaida, ni ngumu sana kwa mwananchi kuvumilia zaidi naye atataka kulizia na ndipo huweka sumu kwenye mzonga na wanyama wengine walao nyama wakala.

Tayari tume maalum imeshafanya uchunguzi na kupendekeza kugawa kanda katika eneo hilo, lakini ni muhimu sana kutoa elimu kwa jamii husika kuelewa ni kwanini lazima wapungue na wapunguze mifugo.

Changamoto kubwa ni ndani ya jamii hiyo waliofanikiwa kusoma kurudi kugeuza mtaji eneo hilo kwa kuwatumia wananchi vibaya kwamba watakuwa na idadi kubwa ya mifugo na kukaribisha wengine, huku kukiwa na taarifa za baadhi ya watu kutumia eneo hilo kama eneo la malisho bila kujali umuhimu wa shughuli za uhifadhi na utalii ambazo zinaliingizia mabilioni ya fedha.

Ni lazima hatua zilichukuliwe kuokoa eneo la Ngorongoro kama raslimali muhimu ya taifa.

Mungu ibariki Tanzania!

**Tutafakari!**



# NI HARUSI YA KALONGA KASATI NA NURU MWAISANGO

iliyofungwa Kanisa la T.A.G Majumba Sita, Desemba 5, 2020 na kufuatiwa na tafrija iliyofanyika Kebby`s Hotel, Mwenge, jijini Dar es Salaam.







# MITINDO





# 'ROLL NECK'
# SWETA LINALOMTOA MTU KIPEKEE

VAZI la sweta la shingo ndefu 'Roll Neck' limekuwa maarufu miongoni mwa vijana, kutokana na mwonekano wake kuwa wa kupendeza zaidi.

Nguo hizi ambazo zinavaliwa sana katika kipindi cha baridi, lakini unaweza kutumia katika kipindi chochote cha majira kulingana na aina ya kitambaa.

Baadhi ya wabunifu wameongeza vionjo na kubadilisha mtazamo na kulifanya vazi hili kuwa chaguo la kipekee pale mtu anapohitaji kutoka kitofauti.

Wanaume wanashauriwa kutumia vazi hili katika shughuli mbalimbali.

UTACHAGUA VIPI?

Endapo unapenda kuvaa nguo ya aina hii, unatakiwa kuhakikisha mtindo na kitambaa kama inaendana na wewe ulivyo.


Unatakiwa kuhakikisha ubora wa kitambaa kwanza, kabla hujaangalia vionjo vingine.

Chagua rangi nzuri na ukubwa unaolingana na mwili wako, kwa sababu ukikosea unaweza kuondoa uhalisia wa mwonekano wako.

Angalia shingo ya sweta kama inanavutika kwa sababu inatakiwa kutanuka na kurudi katika ukubwa wake wa awali. Endapo ukiona inatanuka bila kurudi, basi hiyo sio halisi.

## UREMBO: JICHO NI KILA KITU

# Urembo unaosema wenyewe



MACHO ni moja ya kiungo muhimu kwa kila binadamu kwa ajili ya kuona.

Pamoja na umuhimu huo, macho ni muhimu zaidi kwa wanawake sehemu ya pambo au urembo wake

Pamoja na hayo, kuna aina tofauti za macho ambayo kila mtu amebahatika kuwa nayo, kuna makubwa, madogo, duara na yale ya mkato wa paka.

Hata hivyo, katika aina hizo mtu anaweza kutengeneza macho yake kadri anavyotaka kwa kutumia nyenzo mbalimbali za urembo.

Kama macho yako madogo, unaweza kuyafanya yaonekane makubwa na hata yakiwa na mwonekano wa ukali, ni rahisi kuyafanya yawe yamepooza kama mtu anayesinzia.

**Mahitaji**

Andaa wanja wenye rangi iliyokolea yenye rangi ya kawaida, maskala, pamba kiasi, na kope za bandia.

Jinsi ya kutengeneza macho makubwa

Paka wanja usiokolea kwenye kingo za nje za kope zako, usipake eneo la ndani.

Rudia tena kupaka wanja kwa kukoleza, unaweza kupaka hadi nje kidogo ya kingo za jicho upande wa kulia na kushoto.

Bandika kope za bandia kwa uangalifu, zingatia kope zinakuwa na urefu wa kutosha kwa sababu ndizo zinazopendeza na kufanikisha lengo la kuliweka jicho katika ukubwa mzuri.

Baada ya hapo paka maskala ya kutosha mpaka uhakikishe kope zako zimenyanyuka zaidi.

Naamini kwamba wapo baadhi ya wanawake hawawezi kujitengeneza wenyewe, hivyo usiogope kwenda kwa mtu unayemwamini akusaidie.

## MAPISHI Na Mary Geofrey

# MATOKE YA MBOGA



NDIZI za mboga maarufu kama matoke kwa wanyeji wa mkoa wa Kagera na nchi ya Uganda.

Chakula hiki kinaliwa sana Uganda, na huko unaweza kujifunza namna ya kupika matoke ya aina mbalimbali ikiwamo ndizi zilizosagwa na hazijawekwa kitu chochote na zile zilizochanganywa na mboga.

**Mahitaji:**

Ndizi bukoba kubwa tano, nyanya nne kubwa na ya kopo kijiko kimoja cha chai.

Vitunguu viwili vikubwa, Biringanya mbili, pilipili hoho mbili zilizokatwa vipande vikubwa.

Karoti mbili zilizokatwa vipande, chumvi na mafuta ya kupikia kiasi upendacho.

**Namna ya kupika**

Weka mafuta mafuta, vitunguu kwenye sufuria na anza kuvikaanga ila visiive sana.

Kaanga pamoja adi vitunguu viive, ongeza nyanya ya tunda na nyanya ya kopo, kaanga adi nyanya iive.

Ili kujua nyanya imeiva, nyanya na mafuta vitatengana ndani ya sufuria.

Ongeza ndizi na kaanga kwa pamoja kwa muda adi uone nyanya inashikana na ndizi.

Funika na acha vichemke kwa moto kidogo na baada ya muda huo mimina karoti, biringanya na hoho na ongeza mchuzi.

Hakikisha haziivi sana na ndizi hazikatiki katiki na weka chumvi saizi unayotaka.

Chakula hiki kikiiva kinatakiwa kubaki na mchuzi ambao ni rojo hivyo chakula chako kitakuwa tayari kwa ajili ya kuliwa.

# MAISHA NI NYUMBA

## Na Elizabeth Zaya

# USAFI WA KITANDA NI MUHIMU KWENYE NYUMBA



USAFI wa kitanda ni jambo muhimu linalopaswa kufanywa kila siku katika nyumba.

Pia linaweza likafanywa muda wowote ndani ya siku hiyo moja kwa kutegemea na matumizi ilimradi kionekane kisafi wakati wote na unatakiwa uanze asubuhi unapoamka hadi usiku unapolala.

Usafi ninaouzungumzia hapa ni kuanzia kutandika mashuka, kufuta vumbi katika pande zote zinazokizunguka na kukipangilia vizuri.

Kwa sababu kitanda ni mojawapo ya vitu vinavyofurahisha nafsi kwenye nyumba na kiafya pia, ni vizuri kikapewa kipaumbele kikubwa.

Ni vizuri kukumbuka kuwa, usafi wa kitanda si lazima uhitaji gharama kubwa ni jambo la kujipanga tu kujizoesha na kama ilivyo katika usafi wa vitu vingine, kitanda pia kisipotunzwa vizuri hakiwezi kuwa bora na imara.

Kitu muhimu ni kuhakikisha unakuwa na shuka lako unalotumia kulalia pamoja na unalojifunika, ambalo utalitumia pia katika shughuli hiyo ya kutandika na endapo utaona inafaa zaidi kulingana na uwezo wako, tenga shuka maalum za kutumia wakati wa kulala na za kutandika.

Zipo njia nyingi za kutandika kitanda na mojawapo ni kulitandika katika godoro kwa kuhakikisha limechomekwa ndani na la pili ukalitandika juu na kulikunja kidogo kwa robo ya kitanda au nusu kutoka juu unapoweka kichwa chako kwa kulishusha chini.

Shuka hilo la pili ukiona inafaa likunjie kwa ndani ya godoro au kuliacha kwa nje.

Upande wa chini unapoelekeza miguu wakati wa kulala, weka hata shuka zito ambalo ikiwezekana liwe linafanana na mito yako ili kuongeza mvuto zaidi.

Lakini, kumbuka kwamba usafi katika kitanda chako si lazima uwe na mashuka mengi isipokuwa tu kwa anayehitaji 'kukirembesha' zaidi, kama hauna mengi tumia hilo moja ilimradi liwe safi na mito yako kwa kulitandika kwa ustadi mkubwa.

Kwa sababu utandikaji wa kitanda ni usafi muhimu, pia usisahau kupangilia vizuri mito yako ili kukamilisha usafi zaidi wa kitanda chako na kukipendezesha, jifunze kubadilisha mpangilio wa mito, usipende kutumia wa aina moja.

Kumbuka kila kitu kinahitaji ubunifu, jitahidi kuongeza ubunifu kila siku kutafuta namna bora ya kukifanya kitanda chako kipendeze kwa sababu lengo kubwa ni kuipendezesha nyumba yako, nafsi na ustawi wa afya yako pia.

# MPANGILIO

# DONDOO MUHIMU ZA KUPAMBA NYUMBA YAKO MPYA KABLA YA KUHAMIA

1: Kuwa na bajeti inayokidhi kipato chako


2: Acha kupamba vyumba vyote kwa wakati mmoja, chagua kimoja kwa majaribio ili kuona matokeo yake.

3: Kuwa na orodha ya vitu unavyotaka kununua kwa ajili ya upambaji, hii itakurahisishia kumaliza mapema.

4: Kuwa na muda wa kuangalia maeneo unayoweza kupata vitu kwa haraka na bei nafuu.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
'JANUARWY SPESHO'
JUKWAANI
MIMI KAZI YANGU YA KUKUTIENI MOYO MLIO-KATA TAMAA, MALIPO SIYAPATI KWENU NYIE SIJUI UNANIELEWA?
NINGEKULIPA NINI WAKATI HAPA NILIPO SIPOKEI SIMU YA MWALIMU MKUU WA MWANANGU!
NIMEMPIGIA MWALIMU MKUU KABLA SIJAONGEA KANAMBIA NJOO OFISINI UKIWA KAMILI, SIJUI KAMAANISHAJE?
AFADHALI WEWE UMEPIGA, MWENZIO NIMEPIGIWA KABISA NA 'HEDI MASTA' HAPA NATUNGA 'VESI'
...KUNA BABA MMOJA ALIZAMA KWENYE PENZI LA MCHEPUKO AKASAHAU KUSOMESHA, MATOKEO YAKE WATOTO WAKAWA WEZI NA WAKIKE WAKAWA MAKAHABA... KWA HIYO.... KWAHIYO.....
EMBU RUKA HIYO CHANELI, WEKA 'BONGOFLEVA'
HIVI BABA NANILIU UNAKUMBUKA 'ADA' KAMA USHALIPA?
NITAPATA UHAKIKA AKIRUDISHWA
WENZAKO WOTE KIPINDI HIKI WANA 'STRESS' NA KARO ZA SHULE ZA WATOTO LAKINI NAKUONA WEWE 'UPO NOMO' AU USOMESHI?
STRESS UKIZIENDEKEZA UNAWEZA KUWA MKIWA KATIKA MAPENZI...
BAR
MWALIMU MKUU, MIMI NINAUMWA MOYO. TAIFODI, KISUKARI, PRESHA VIDONDA VYA TUMBO, YUTIAI KISONONO NA NILIFANYIWA OPARESHENI YA KOO JUZI JUZI...HELA YOTE IME-ISHIA HUKO!...
NDIO MAANA SAUTI YAKO INASIKIKA VIZURI KAMA SABUFA MPYA.... LAKINI MWANAO KAMA HANA ADA ASITIE KWATO ZAKE HUKU...
AU...NJOO NA VYETI VYOTE VYA DAKTARI... UNAVYO?
NITAVITAFUTA ILA NYUMBA YANGU INA PANYA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...PONDA RAHA LEO.... USIKILIZIE MAUMIVU KESHO

# Twitter yamfungia Rais Trump

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amefungiwa akaunti yake ya Twitter, baada ya kuwapo kwa ujumbe kadhaa zinazohatarisha kuchochea vurugu miongoni mwa raia wa nchi hiyo.

Kampuni ya Twitter, ilisema katika taarifa yake kuwa uamuzi huo umefikiwa baada ya kufuatiliwa kwa karibu kwa ujumbe wa Twitter wa akaunti ya @realDonaldTrump account" ambayo inamilikiwa na kiongozi huyo.

Kumekuwapo kwa wito kutoka kwa baadhi ya wabunge na watu mashuhuri, kwa kampuni za mitandao ya kijamii kuzifunga akaunti za Trump, kutokana na jumbe zake kuibua hisia kwa jamiii.

Aliyekuwa mke wa Rais Barack Obama, Michelle Obama, aliandika ujumbe kwenye Twitter, Alhamisi akiomba kituo cha ubunifu wa teknolojia duniani, Silicon Valley, kuzuia uendelezaji wa tabia mbaya za Trump na kumfuta kabisa kama mtumiaji wa huduma hizo.

Trump alifungiwa akaunti yake ya Twitter kwa kipindi cha saa 12 Jumatano baada ya kutoa wito kwa wafuasi wake kuvamia jengo la Bunge Capitol Hills.

Mtandao wa Twitter baadaye ikarudisha mawasiliano na kaonya wanaweza kumfungia kabisa ikiwa atakiuka tena kanuni za jukwaa hilo la mawasiliano.

Hata hivyo, baada ya kurudishwa hewani Rais Trump, alituma ujumbe kwenye mtandao wa Twitter juzi akisema kampuni hiyo ilikuwa mwisho wake kuchochea.

Kisha alituma ujumbe mwingine unaosema "Wamarekani 75,000,000 wazalendo walionipigia kura, Marekani Kwanza na Fanya Marekani kuwa Bora Tena, watakuwa na sauti inayosikilizwa siku zijazo. Hawatakosewa heshima au kuchukuliwa kwa uonevu kwa namna yoyote ile!!!"

Hata hivyo, Mtandao wa Twitter ulisema ujumbe huo unatafsiriwa kama ishara kiongozi hiyo hana nia ya kuhakikisha kunafanyika makabidhiano ya madaraka kwa njia ya amani.

Mtandao huo uliongeza kusema kuwa katika ujumbe wote alioandika unakiuka sera na kanuni.

Baada ya akaunti hiyo kufungiwa, Rais Trump, alituma ujumbe mwingine kwa kutumia akaunti rasmi ya rais wa Marekani @Potus akisema ataangalia uwezekano wa kuwa na mtandao wao utakaowezesha kuwa na mawasiliano siku za usoni.

Hata hivyo, ujumbe huo ulifutwa haraka katika jukwaa hilo la mawasiliano muda mfupi baada ya kuwekwa.

**BBC**




Raia wa Ethiopia, akiwasili na kitanda chake katika kambi ya wakimbizi ya Tenedba iliyopo mashariki ya Sudan baada ya kukimbia mapigano katika jimbo la Tigray juzi. **(PICHA: AFP)**

# Korea Kaskazini kuimarisha silaha za kinyuklia

**PYONGYANG, Korea Kaskazini**

KIONGOZI wa Korea Kaskazini, Kim Jong-un, ameitaja Marekani kuwa adui wake mkubwa na kwamba hatarajii nchi hiyo kubadilisha sera yake ya kuimarisha silaha za nyuklia, bila kuangalia nani ataongoza nchi hiyo.

Akizungumza katika kikao cha chama chake tawala cha Workers' Party, Kim aliahidi kupanua mpango wake wa silaha za nyuklia na uwezo wa kijeshi.

Alisema mipango ya utengenezaji nyambizi za nyuklia iko karibu kukamilika.

Matamshi hayo yanakuja wakati Mteule Joe Biden, anajitayarisha kuingia madarakani Januari 20 mwaka huu.

Wachambuzi walisema maneno ya Kim ni kuzidisha jitihada zake za kuongeza shinikizo kwa rais mteule wa Marekani kurudi katika meza ya majadiliano.

Kim alifurahia uhusiano mzuri kati yake na Rais Donald Trump, ambaye anaondoka madarakani, ingawa kulikuwa na hatua ndogo ya kupata suluhu kuhusu mpango wake wa nyuklia.

Katika hotuba yake ya hivi karibuni, Kim alisema Korea Kaskazini, haina nia ya kutumia silaha zake za nyuklia pengine pande hasimu ziwe zinapanga kutumia silaha hizo dhidi ya nchi yake.

Kim alisema Marekani imekuwa kikwazo kikubwa kwa mapinduzi yao na adui yao mkubwa.

"Haijalishi ni nani atakayekuwa madarakani, uhalisia wa sera yake dhidi ya Korea Kaskazini hautabadilika," Shirika la habari la KCNA lilimnukuu kiongozi huyo.

**BBC**

# Iran yakataa chanjo kutoka Marekani

**TEHRAN, Iran**

KIONGOZI mkuu wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei, amepiga marufuku uingizwaji wa chanjo ya Covid-19 kutoka kampuni na Uingereza.

Chanjo zilizopigwa marufuku ni Pfizer ya Marekani, BionTech na Astrazeneca kutoka Uingereza baada ya kuzitaja kutokuwa na imani nazo.

Katika hotuba aliyoitoa kupitia vyombo vya habari, Khamenei, alisema nchi yake haitoagiza chanjo hizo kutoka Marekani na Uingereza, akihofia idadi ya vifo vinavyoendelea kusajiliwa katika mataifa hayo.

Aidha, kiongozi huyo amedai kwamba mara nyingine mataifa hayo yamekuwa yakitaka kufanya majaribio ya chanjo zao kwa watu wa mataifa mengine.

Kiongozi huyo alikubali kuingizwa kwa chanjo kutoka mataifa mengine salama na anaendelea kuunga mkono juhudi za Iran kutengezeneza chanjo yake ambayo tayari inafanyiwa majaribio tangu mwezi Desemba mwaka jana na inatarajiwa kuanza kuuzwa hivi karibuni.

**DW**

# Sassou Nguesso kugombea tena Congo

**BRAZZAVILLE, Congo**

RAIS Denis Sassou Nguesso, ametangazwa na chama chake kuwa mgombea wake katika uchaguzi mkuu utakaofanyika mwezi Machi mwaka huu.

Kiongozi wa Kamati Kuu ya Chama cha Congolese Party of Labour (PCT), Esther Ayissou Gayama, alisema kikao cha kamati hiyo kimeridhia uteuzi wa Sassou Nguesso kwa kura nyingi.

Sassou Nguesso, mwenye umri wa miaka 77, amekuwa madarakani kwa miaka 36, tangu alipochaguliwa kuwa rais mwaka 1979, na kumfanya kuwa miongoni mwa viongozi waliodumu kwa muda mrefu madarakani.

Mwaka 2015, nchi hiyo iliandaa kura ya maoni juu ya kuondoa sheria ya ukomo wa miaka 70 kwa wagombea wa urais, pamoja na kuondoa sheria inayopinga rais kuhudumu kwa zaidi ya mihula miwili.

**DW**

MAKALA

# Namshukuru mama yangu



Na Magabilo Masambu

**Mfano mdogo tu, mtoto anapofanya kosa nyumbani, mama yake anamwambia ngoja baba yako arudi. Baba ukifika unaelezwa makosa ya mtoto, unachukua kiboko unamchapa. Ukitega mgongo tu mama anajipa kazi ya kubembeleza.**

NAMSHUKURU mama yangu. Ndilo neno linalosikika mara nyingi zaidi kwa watu wengi wanapoeleza walivyofanikiwa katika maeneo mbalimbali, hasa kimaisha. Neno namshukuru baba yangu, halijawahi kuwa jepesi kutamkwa na wengi. Hali hii imenisukuma niandike makala hii.

Katika makala iliyopita, niliandika zaidi kuhusu fadhila za watoto kwa wazazi wao. Nikaeleza mafanikio yalivyo na njia nyingi na kwamba fadhila lazima ziwe na pande mbili. Leo nazungumzia upande wa wazazi hawa wawili.

Jean Piaget (1896-1980) katika kitabu chake cha Human Development and Psycholgy anaeleza kuhusu tabia za watu zinakotoka. Moja ni tabia za kibaolojia hapa inahusisha tabia za kurithi kutoka kwa wazazi wawili. Pili ni kutokana na mazingira.

Nitajikita katika tabia za kimazingira maana ndizo zina nafasi kubwa katika hili nalolizungumzia japo kibailojia pia bado inampa nafuu mama kujenga upendo pindi tu mimba inavyotungwa. Mazingira yanachukua nafasi kubwa zaidi.

Kisaikolojia, watoto wanajenga upendo mkubwa kwa watu walio karibu na wanaowanyesha upendo katika umri mdogo. Kwa hiyo ikitokea ukazaa watoto, kisha wakalelewa na watu wengine, basi mapenzi yao kwa watu hao yatakuwa makubwa zaidi kuliko kwako. Kumzaa tu mtoto haitoshi kumfanya akupende bali upendo ni matokeo ya uhusiano wa kila siku.

Hapa ndipo wanaume wengi tunapokwama na kuwafanya kinamama wajichukulie ushindi wa mezani usiostahili. Watoto wasipokupenda ututoni hawatakupenda ukubwani. Mtume Petro ametuasa wanaume tuishi na wake zetu kwa akili na kwamba mwanamume ni kichwa na akili hukaa kichwani. Wanachotuzidi wanawake ni ujanja.

Mfano mdogo tu, mtoto anapofanya kosa nyumbani, mama yake anamwambia ngoja baba yako arudi. Baba ukifika unaelezwa makosa ya mtoto, unachukua kiboko unamchapa. Ukitega mgongo tu mama anajipa kazi ya kubembeleza. Ni jambo dogo lakini lina maana kubwa sana katika kuharibu uhusiano kati ya baba na mtoto huyo, maana yake unakuwa kama uchonganishi na kumfanya mtoto amuone baba ndiye mbaya.

Eneo la pili kubwa kabisa ni namna tunavyohudumia familia kuanzia chakula, mavazi mpaka ada ya shule. Unakuta baba ndiye anayehangaika kutafuta vyote hivi. Kosa kubwa tunalofanya wanaume ni kukabidhi kila kitu kwa mwanamke chumbani. Pesa ya chakula, mavazi na ada unampatia halafu yeye anakwenda kufanya.

Si jambo baya, lakini wanaume tambueni hili ni kosa la kiufundi, ambalo hutaona madhara yake leo subiri watoto wafanikiwe ndio utajua kwanini pimbi alikosa mkiwa, ikiwa mjomba yake ndiye aliyekuwa akigawa.

Mama anakwenda sokoni, mnadani anawapikia chakula na kuwavalisha nguo alizokwenda kuwanunulia kwa pesa ulizompatia kisha watoto wanamwambia mama asante kwa chakula na nguo. Wewe ukirudi unakutana na mashtaka unaweka bakora ukitoka kama kawaida nyamaza mwanangu hata mimi sikupenda baba yako akuchape! Shtuka.

Eneo la tatu ni juu ya mtazamo. Tunatofautiana katika kuyaona mambo japo nia inakuwa njema. Mfano baba anataka mtoto asome awe fulani, mtoto hataki kusoma anataka kuimba au kuchekesha.

Inawezekana mafanikio yake yako hapo kama nilivyoeleza katika makala iliyopita. Baba anamkatalia si kwa ubaya, mama anampa moyo kesho mtoto anafanikiwa kisha anasema bila mama yangu nisingefika hapa. Badala ya mtoto kufikiri kwamba baba hata baba yake alikuwa na nia njema naye asome, anabaki anamlaumu.

Eneo la nne ukaribu. Hapa wanaume tunaweza kulaumiwa bure. Tumeumbwa kuhangaika na vitu zaidi kuliko watu. Fanya utafiti, ukikuta watoto wadogo wanacheza simama tazama, utaona watoto wa kiume wanahangaika na matofali, mara agongelee msumari kwenye mbao na kadhalika.

Wakike utaona anabeba magunzi mgongoni akibembeleza, kujipikilisha na kuigiza kama ananyonyesha hii ni asili. Upendo wetu mkubwa uko kwenye vitu, matrekta, miti na kadhalika. Tubadilike, tuonyeshe upendo kwa watoto wetu pamoja na changamoto za utafutaji. Tuwe na muda wa kukaa nao. Kama ni nguo, ada, chakula fanya waziwazi tusiwape wanawake ushindi wa mezani kisha tuishi kwa tabu uzeeni.

Mwisho, Wizara ya Katiba na Sheria inahitaji kutazama upya sheria inayompa mamlaka mwanamke kubaki na watoto mpaka umri fulani pindi wanandoa wanapoachana. Hii inaweza kuwa sababu kubwa ya wanaume wengi kutowatunza watoto kwa kuona kwamba anaendelea kumuhudumia mtalaka wake. Hivyo anaamua kuacha kutoa huduma kwa watoto.

Nashauri kuwe na mazungumzo ya wanafamilia kukubaliana watoto walelewe na nani. Mbona ikitokea mwanamke kafariki dunia na kuacha watoto wadogo, sheria imekaa kimya kuhusu nani atalea watoto hao? Badala yake watoto hulelewa na ndugu upande wa mume kwa makubaliano ya kifamilia. Kimsingi kwa utamaduni wetu watoto ni wa baba.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Kipindi cha 'Kumekucha' kilivyowakera wanafunzi



Na Adam Fungamwango

**Kwa wafanyakazi, yaani waliokuwa watu wazima wakati huo, kwao wala haikuwa shida, lakini shughuli ilikuwa kwa wanafunzi, kwani utoto bado ulikuwa unasumbua. Kuamka alfajiri hadi kwa wanafunzi wa leo ni tatizo kubwa. Mara nyingi wazazi hutumia mbinu za kuwaamsha watoto ili waende shuleni.**

KUMEKUCHA sasa kumekucha, majogoo vijijini yanawika, hata na jua mbinguni linatoka, wazalendo amkeni tufanye kazi sasa..."

Huu ni wimbo maarufu sana kuanzia katikati ya miaka ya 1970 hadi katikati ya miaka ya 1990. Umaarufu wake hasa ulikuwa ni kwa wanafunzi wa wakati huo. Hakuna mwanafunzi yeyote wa miaka hiyo ambaye haufahamu wimbo huu.

Ni wimbo uliopigwa na bendi ya Safari Trippers, ukitungwa na Jabali la Muziki, Marijani Rajabu, ambaye ametangulia mbele za haki.

Sidhani kama kuna mwanafunzi yeyote wakati huo aliyekuwa anajua wimbo huu umepigwa na bendi gani au mtunzi, au aliyetaka kujua hilo.

Ni kwa sababu wengi walikuwa hawaupendi. Wala haukuwa wimbo mbaya, ulipigwa vibaya au mwimbaji wake hakuwa mahiri kwenye uimbaji, la hasha. Huu ni wimbo ambao ulikuwa ukipigwa redioni majira ya kuanzia saa 11:30 hivi na ndiyo uliokuwa ukitambulisha muda kuwa sasa ni wakati wa kuamka na kwenda shuleni.

Wimbo huo ulikuwa unapigwa kuashiria kuanza kwa kipindi kilichokuwa kinaitwa 'Kumekucha' ambacho kilichukiwa tu na wanafunzi kwa sababu kiliwekwa muda ambao walikuwa wanatakiwa waamke kwenda shuleni.

Mwanafunzi yeyote yule wakati huo akiusikia wimbo huo kama amelala, basi tayari kwake ni ishara kuwa aamke mara moja na kufanya maandalizi ya kwenda shuleni, jambo ambalo kwa wanafunzi wengi ilikuwa shida kwani ni wakati ambao usingizi unakuwa mtamu sana.

Kwa wafanyakazi, yaani waliokuwa watu wazima wakati huo, kwao wala haikuwa shida, lakini shughuli ilikuwa kwa wanafunzi, kwani utoto bado ulikuwa unasumbua. Kuamka alfajiri hadi kwa wanafunzi wa leo ni tatizo kubwa. Mara nyingi wazazi hutumia mbinu za kuwaamsha watoto ili waende shuleni.

Burudani inakuja kipindi cha baridi kali au siku za mawingu au mvua, halafu denti kajifunika shuka gubigubi, masikio yake yanakutana na wimbo huo.

Ikumbukwe zamani redio ilikuwa ni moja tu, Radio Tanzania Dar es Salaam, hivyo haikuwa rahisi kukwepa kuusikia.

Hata kama mzazi wako hakuwa na redio, lakini hata unaweza ukaisikia kwenye nyumba ya jirani.

Ni wakati ambao mwanafunzi anatakiwa aamke haraka ajiandae na kwenda shule kuwahi namba. Kumbuka kama hukupata namba, unahesabika kuwa umechelewa. Na mara nyingi wakati huo, namba zilikuwa zinahesabiwa saa 12:00 asubuhi.

Sasa unaweza kuusikia wimbo huo, ukaamka kwa kujivutavuta au ukaamshwa kwa nguvu na mlezi au mzazi, ukajiandaa na kuondoka nyumbani. Lakini inategemea pia umbali wa nyumbani na shule pia. Njiani unaweza kuusikia tena wimbo huo huo ukiimbwa.

"Sasa kaziii, oooo mama, ooo mama ooo, sasa kaziii, acha mchezo na kazi, ooo mama..." Ukisikia hivyo kwenye redio kama uko njiani kwenda shule, ujue umechelewa namba. Sasa ni hiari yako, uharakishe uende ubahatishe labda siku hiyo wamechelewa kidogo kuhesabu namba, au uamue kutembea taratibu kwa sababu hakuna faida tena ya kuharakisha, na bakora ya uchelewaji zitakuwa zinakusubiri.

Ni kwamba ukisikia kipande hicho, ni kwamba kipindi cha 'Kumekucha' ndiyo kinamalizika. Na inakuwa ni saa 12:00 za asubuhi. Ni muda ambao mwanafunzi alitakuwa awe ameshafika shuleni.

Hii ndiyo sababu kubwa iliyosababisha kipindi hicho cha 'Kumekucha' kichukiwe mno na wanafunzi wengi wakati huo kutokana na kuwekwa kwenye wakati ambao kunakuwa na mchakato wa wao kuamka na kwenda shule.

Ukiachana na kipindi hicho, kipindi kingine ambacho hakikuwa rafiki kwa wanafunzi, bali watu wazima ni 'Mashairi'. Mghani maarufu wa wakati huo ni Athumani Khalfan. Ni kipindi kilichopendwa na watu wengi, hasa watu wazima.

Wanafunzi wengi walikuwa hawakipendi kwa sababu nacho kilipata bahati mbaya ya kuwekwa mida ya saa saba hadi nane, kipindi ambapo zamani ndiyo muda wa wanafunzi kurudi majumbani.

Ni kipindi ambacho wanafunzi wengi wanarejea wakiwa na njaa, hivyo njiani wakisikia mzee huyo akighani mashairi, wao akili yao iko kufika nyumbani upesi ili wapate chakula.

Kwa bahati mbaya sana unaweza kurejea nyumbani ukakuta siku hiyo yamepikwa maharage yaliyoiva upesi hadi yatiwe magadi, na ukiendelea kusikia mashairi yale, unatamani kulia.

Kuna mtu mmoja aliniambia kuwa yaani yule mzee kila anapobadilisha aina ya sauti ya kughani njaa, ndiyo inazidi.

Hapa tatizo si kwamba mashairi au sauti ile inasababisha njaa, ila wanafunzi tayari walishakariri muda wa saa saba mpaka nane ulikuwa ni wa kurudi nyumbani na ni kweli ulikuwa muda ambao njaa inakuwa inawauma. Na ubongo wao tayari unakuwa umeshaakisi kitu kama hicho.

Nadhani kipindi kile kingewekwa saa tisa au kumi wakati wameshiba, wala kisingekuwa kinachukiwa.

Hadi leo hii wakati wengi wa wanafunzi hao wameshakuwa watu wazima, wakiwa sehemu yoyote ile na yakasomwa mashairi, basi wataangaliana, watatabasamu, watacheka na kila mmoja atakwambia kuwa anakumbuka wakati huo akitoka shule njaa inamuuma.

Mwingine anaweza hata kutania kuwa amesikia mashairi hayo yanasomwa, basi njaa imeshaanza kumuuma.

# HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora jijini Dar es Salaam. Sauti hizo za risassi zilifanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu. Haikuwa hivyo. Aliyedhaniwa kuwa ni jambazi alichofanya ni kumpora mwanamke mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja tu na kuondoka naye akiwa kwenye gari aina ya IST. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini aliyemteka mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji? Fuatilia kisa hiki kitamu, cha kusisimua na kuhuzunisha.

# Nina jambo langu-4

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

HAYO ni mawazo ya Jerry aliyokuwa akiyakumbuka kutokea kiasi cha miezi minne iliyopita.

Alichokiona ndicho kilichomkumbusha yote hayo. Baada ya kupiga picha gari ambalo aliyemteka mtoto wa Neema aliondoka nalo, aliamua kushuka chini kwa kutumia ngazi kwa kasi.

Alitaka kwenda kuchukua gari lake alilopaki, lakini akabadili mawazo ghafla. Alijua mbele ya safari anaweza kukwama kutokana na foleni kubwa kwenye makutano ya barabara ya Kawawa na Nyerere maeneo ya Keko Veta.

Akataka kukimbilia kwenye kituo cha bodaboda, lakini kabla hajafika, kuna bodaboda moja ilikuwa ikitokea Chang'ombe na kukata kona kuelekea Uwanja wa Benjamin Mkapa, akaipungia mkono.

Mwendesha bodaboda akageuza. "Unaweza kuendesha kwa mwendo wa kupaa?"

"Hilo tu mwanangu, bora useme lingine." Alijibu kijana huyo kwa kujiamini huku akitabasamu.

Wakati akijibu, tayari Jerry alikuwa ameshadanda kwenye kiti cha abiria.

"Nataka ukimbie haraka, kuna gari moja nalifuata, nitakuonyesha kama tutafanikiwa kuliona."

"Gari la aina gani?" Aliuliza.

"Ni hivi, wewe endesha, mimi nitakapoliona nitakwambia kama ni lile, halafu baada ya hapo utafuata maelekezo yangu."


"Malipo?"

"Usijali, nitakulipa utakachohitaji." Jerry alimjibu na wakati huo huo, bodaboda ikichanja mbuga kuelekea maeneo ya Keko anapouza vitanda, viti, meza na vitu vingine vya ndani.

Kwa umbali mrefu hakuweza kuliona gari lolote lililofanana na lile. Hata hivyo, kwenye makutano ya barabara ya Nyerere na Kawawa, aliona gari inayofanana na ile ikikata kona kushoto ikielekea maeneo ya Uwanja wa Ndege.

"Kata kushoto." Alimuamuru mwendesha bodaboda. Akatii.

Wakati anakaribia kufika kwenye makutano ya barabara na Nyerere na Mandela, aliliona tena gari lile. Lilikuwa limesimama kwenye foleni. Walipokuwa wanakaribia likasogea kwenye foleni, likakata kulia na kuelekea Buguruni.




**"Mimi haiingii akilini. Isijekuwa ni bwana 'ako, alikuwa anakudai mtoto, akaamua kufanya hivyo?" Hatimaye Ben akatapika nyongo. "Unanitukana ee baba Diana. Yaani umefika sehemu ya kuniona mimi ni mwanamke na kujitembeza huko, halafu nimepata mimba nimekuletea wewe na sasa wananidai mtoto kweli?" Neema alianza kulia.**

Ni wakati ambapo Jerry aliziona namba za gari hilo. Ili kuthibitisha kuwa kweli ni lile, alitoa simu yake ya mkononi na kutazama picha alizolipiga gari lile wakati wa tukio kule Keko.

Alibonyeza kitufe cha kuzivuta picha zile ili gari lionekane kwa karibu zaidi. Akasoma namba na akabasamu.

Ndiyo. Gari alilokuwa akilitafuta na kulifukuzia ndiyo lile. Sasa lilikuwa limepita Buguruni likielekea maeneo ya Tabata.

"Gari nililokuwa linalisaka ni lile pale mbele. IST ya rangi ya maziwa. Sasa cha kufanya punguza mwendo, twende taratibu. Likisimama kwenye foleni sisi tunalipita halafu mbele tunakaa pembeni kama kuna kitu hakiko sawa hivi, halafu likiondoka na sisi tunalifuata. Nataka kujua tu mwisho litafikia wapi."

"Sawa braza hakuna tatizo, pesa yako tu."

"Pesa haina shaka, ila tahadhari ni kwamba tunayemfuata asijue."

"Unaenda kufumania nini?"

"Siyo kazi yako."

Ilikuwa ni safari na muda mrefu kidogo, lakini mwisho wake ni kwamba Jerry alishuhudia kwa macho yake, gari lile likiingia kwenye nyumba moja maeneo ya Ubungo Maziwa.

Lilikuwa ni jumba la kifahari. Hakumshuhudia mtoto wala mtu aliyemteka. Alichoona ni gari lile likifika nje ya geti la jumba hilo. Likafunguliwa na gari ikazama ndani. Geti likafungwa na ukawa mwisho wa mchezo.

Ili wasishtukiwe kama kuna kitu walikifuata, alimuamuru dereva wa bodaboda kutogeuza, badala yake waendelee mbele na barabara hiyo hiyo ya mchanga ili mbele watafute njia nyingine ya kurejea kwenye barabara kuu.

Kitu pekee ambacho alichoondoka nacho na cha muhimu kwake ni kuwa na uhakika kuwa gari lililombeba mteka mtoto na mtoto mwenyewe, limeingia kwenye nyumba hiyo.

****************************

"Mama Diana naomba unijibu maswali yangu tafadhali. Yule jamaa aliyekupora mtoto unamfahamu au humfahamu?"

"Ni kwambie mara ngapi mume wangu, mimi simfahamu."

"Hivi, watoto wako wangapi hapa Dar es Salaam. Kwanini atoke kote huko aje kupora mtoto huyu tu mmoja?"

"Hapo hata mimi sijui kwa kweli."

Ulikuwa ni mzozo. Mzozo ambao umezuka kwa Neema na mumewe Benson.

Ben alikuwa na mawazo tele kichwani. Achana na kutokuwa na uhakika wa maisha ya mtoto na dhamira ya mtekaji, lakini alichokuwa akijiuliza ni kwa nini awe yule tu si mwingine?

Akili ikaenda mbali zaidi na kudhani kuwa huenda mkewe anamfahamu mtekaji. Kama si hivyo mkewe kuna kitu amefanya ambacho hakifahamu ndicho kimesababisha mtoto atekwe.

"Mimi haiingii akilini. Isijekuwa ni bwana 'ako, alikuwa anakudai mtoto, akaamua kufanya hivyo?" Hatimaye Ben akatapika nyongo.

"Unanitukana ee baba Diana. Yaani umefika sehemu ya kuniona mimi ni mwanamke na kujitembeza huko, halafu nimepata mimba nimekuletea wewe na sasa wananidai mtoto kweli?" Neema alianza kulia.

Neema alilia na mengi. Kwanza hajui hatima ya mtoto wake. Kwa siku ya pili sasa, amelala wapi. Anaishi vipi? Anakula wapi. Yuko hai au? Hii ilikuwa inamfikirisha na kumkosesha raha na kulia mara kwa mara, licha ya kwamba tayari wameshapiga ripoti kwenye kituo cha polisi Keko.

Sasa imekuja hii ya mumewe kutoamini kama ni utekaji wa kawaida au una makandokando ya mapenzi nyuma yake.

Neema anaamini kuwa hakuna kitu kama hicho, kwani hakuwahi kuwa na mpenzi yoyote jijini Dar es Salaam tangu akaingia akitokea Mbeya.

Na hata huko Mbeya, alikuwa na mpenzi ambaye hakuwa anatembea naye kizembezembe hadi kupata ujauzito.

Alipoingia Dar alikutana na Ben na kuishi kwa mwaka mmoja tu kabla ya kufunga ndoa.

"Usilete mkosi baba Diana. Hapa yenyewe hatujui hatima ya mtoto. Nimeumia sana mimi, nalia usiku kucha, wewe nawe unazidi kuniumiza."

Ben alijua amekosea. Lakini hakuwa na la kusema wala la kufanya. Ujumbe ulikuwa umefika.

Neema alikuwa anahitaji kujua hatima ya mtoto wake Diana. Ben hakutaka kujua hatima tu. Alitaka kwenda mbali zaidi. Hata kama atapatikana akiwa hai, lakini alitaka kwenda zaidi ya hapo. Alitaka kujua kwa nini alitekwa. Kwa nini alitekwa yeye akiwa ndani ya mamilioni ya watoto waliopo Dar es Salaam. Nani aliyemteka? Na ana uhusiano gani na mtoto huyo, pamoja na mama yake?

**INAENDELEA JUMAPILI**



# UTAMJUAJE PILI KITIMTIM?

MCHEKESHAJI Pili Kitimtim, amewaambia watu wanaodhani anaishi kwa pesa za wanaume waache mara moja, kwani ana pesa kiasi ambacho anaweza kununua gari la Sh. milioni 35.

Akizungumza na EATV, Pili Kitimtim amesema kwa kawaida hamchuni mwanaume wake pesa wala halipiwi kodi na matumizi mengine, ila anachotegemea kutoka kwa mpenzi wake huyo ni furaha mawazo na kushauriwa.

"Mimi na mpenzi wangu tunashindana kiuchumi, kwenye gari zangu zote tatu hajatia hata elfu tano zake, hanilipii kodi na mimi simlipii kwa sababu wote ni vijana tunatafuta na hatuchunani, kwenye mahusiano yetu gari ni kitu cha kawaida kama ni Sh. milioni 35 kwangu ni kitu cha kawaida nanunua," amesema Pili Kitimtim.



# BEN POL APINGA KUJIKOMBA

MWANAMUZIKI wa miondoko ya R&B nchini, Ben Pol, amesema ukaribu wake na wasanii wa Marekani, ni jambo la kawaida na kamwe hawezi kujirahisisha.

Ben Pol, amesema huenda watu wanahisi anachezea nafasi kwani mpaka hivi sasa hakuna kinachoendelea licha ya kuwa na urafiki na wasanii wa Marekani pamoja na mwanasoka Depay

"Sio kila mtu wa kumtumia kutunza watu, ni jambo zuri sana utakapoenda kwa lengo la kumtumia, lakini ndio mwanzo wa kuanza kuwapoteza watu hao ambao ni muhimu zaidi kwenye maisha," amesema Ben Pol.

# ASHA BOKO KUMBE ANAPENDA VIMBAUMBAU

MSANII wa filamu za vichekesho, Asha Boko, ameamua kutaja siri zake, baada ya kueleza ugonjwa wake ni wanaume wembamba.

Asha Boko amesema hayo jana baada ya mashabiki wengi kuhoji umri wa mume wake mpya ambaye anaonekana kuwa mdogo kwake.

"Mume wangu nipo naye miaka miwili iliyopita, ila ni wembamba wa reli na sio kusema kwamba ni mdogo halafu mimi wanaume wembamba ndiyo ugonjwa wangu, umri wangu au wake haiwahusu wajue tu ni mkubwa wala sio mtoto. Kwanza hata marehemu mume wangu wa kwanza kimwili chake kama huyu wa sasa," amesema Asha Boko.



## HABARI MICHEZO




# SOLSKJAER

## KUTEMA WAWILI UNITED

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amethibitisha atawatema wachezaji wawili wa kikosi chake.

Wachezaji hao ni Marcos Rojo na Sergio Romero ambao wameruhusiwa kuondoka pale United.

Rojo na Romero hawana namba kwenye kikosi cha United na Solskjaer amethibitisha kuwaruhusu wachezaji hao kuondoka katika dirisha hili la usajili mdogo wa Januari.

Akizungumzia uwepo wa wachezaji hao kwenye kikosi chake, Ole amesema, "wote (Rojo na Romero) wana mikataba mpaka mwisho wa msimu, lakini mikataba yao haitoongezwa, tumewaruhusu kutafuta klabu nyingine."

Rojo anapata wakati mgumu kupambania namba na Erick Bailly, Harry Maguire, Victor Lindelof, Luke Shaw, Alex Telles na Axel Tuanzebe.

Romero amejikuta akishuka namba na kuwa kipa namba tatu nyuma ya David De Gea na Dean Henderson.

# WENGER NAYE ATAJWA INTER MIAMI

**LONDON, England**

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger ameunganishwa na Phil Neville kuwania kibarua katika klabu ya Inter Miami inayoshiriki Ligi Kuu Marekani, imeelezwa.

Safari ya Inter Miami kumsaka kocha mpya baada ya kumalizana na Diego Alonso inaendelea kunoga, orodha ikiendelea kupamba huku makocha wazoefu na waliopata mafanikio makubwa katika soka, wakipewa kipaumbele.

Kwa mujibu wa ripoti za soka, kocha anayeachana na timu ya taifa ya wanawake ya England, Neville ndiye anayepigiwa upatu zaidi kuwa kwenye mazingira mazuri na kibarua hicho.

Hata hivyo, Inter Miami ambao wanashiriki Ligi ya MLS wanaendelea kutazama kocha bora atakayewafaa na wana machaguo kadhaa mezani, Wenger, Robbie Keane na Bob Bradley wakiwa kwenye orodha.

Neville ambaye anaonekana kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi anatajwa kuwa anatazamia kumalizia jukumu lake kwenye timu ya taifa.

Kuna taarifa kuwa licha ya kuwa Neville anataka kuondoka kwenye timu ya taifa ya wanawake ya England, huenda tofauti zake na Shirikisho la Soka zikamalizika na akasalia na kibarua chake, hii inamaana Wenger, Robbie Keane na Bob Bradley wanakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi.





## SIKU ZA LAMPARD ZINAHESABIKA

**LONDON, England**

KIBARUA cha Kocha wa Chelsea, Frank Lampard, kimeingia kwenye wakati mgumu baada ya uongozi wa timu hiyo kuanza mikakati ya kusaka kocha mpya wa kushika nafasi yake.

Timu hiyo imekusanya pointi nne tu katika mechi sita zilizopita za Ligi Kuu England.

Taarifa kutoka vyanzo mbalimbali zinadai mabosi wa Chelsea tayari wameanza mchakato wa kusaka mbadala wa Lampard kutokana na kile kinachodaiwa kutoridhishwa na matokeo wanayopata pamoja na ufanisi wa timu.

Katika mechi sita zilizopita, Chelsea imeshinda moja dhidi ya West Ham, imetoka sare dhidi ya Aston Villa huku ikipoteza dhidi ya Everton, Wolves, Arsenal na Manchester City.

Lakini kana kwamba haitoshi, mchango wa nyota wapya waliosajiliwa kwa fedha nyingi baada ya mapendekezo ya Lampard, Kai Havertz na Timo Werner umekuwa duni tangu walipojiunga na timu hiyo.

Wener aliyenunuliwa kwa ada ya pauni milioni 47.5 (sawa na Sh. bilioni 150 za Tanzania) hajaifungia Chelsea bao lolote katika mechi tisa mfululizo za Ligi Kuu England zilizopita licha ya kufunga mabao 28 katika mechi 34 alizoichezea timu yake ya zamani RB Leipzig msimu uliopita.

Naye Kai Havertz ambaye alinunuliwa kwa dau la pauni milioni 89 ameifungia Chelsea mabao mawili tu huku akiwekwa nje ya kikosi cha kwanza katika mechi nne za Chelsea kwenye Ligi Kuu England.

Taarifa hizo zinadai kuwa uongozi wa Chelsea umeanza kuwa na shaka na hali ya baadaye ya timu yao chini ya Lampard na wanadhani kuwa huu ni wakati sahihi wa kutafuta mtu wa kuongoza jahazi lao hapo baadaye.

Kati ya majina ambayo yamekuwa yakihusishwa zaidi kuchukua nafasi hiyo ya Lampard ni kocha aliyetupiwa virago na PSG, Thomas Tuchel ambaye pia aliwahi kuinoa Borussia Dortmund.

Lakini wakati joto likizidi kupanda kwa upande wake, Lampard alisema kwa sasa akili yake ameielekeza katika kuhakikisha timu inarudi katika mstari na suala la kutimuliwa au kubaki, halitilii maanani.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# POCHETTINO AMTAKA AGUERO ATUE PSG

●●● Tayari mshambuliaji huyo hajaonyesha nia ya kusaini mkataba mpya na City na kujiweka katika...

**PARIS, UFARANSA**

KOCHA mpya wa Paris Sint Germain, Mauricio Pochettino, anaripotiwa kuwa anamtupia jicho nyota wa Manchester City, Sergio Aguero kwenye malengo yake ya kumsajili kama mchezaji huru.

Nyota huyo ambaye amekuwa kinara wa magoli pale City kwa wakati wote anakaribia kufika tamati kwenye mkataba wake wa sasa na bado hajaonyesha dalili za kusaini mkataba mpya mapema.

Aguero kwa sasa ana uwezo wa kufanya makubaliano ya awali na timu yeyote ya nje kuelekea kwenye uhamisho wake huru ifikapo Julai, mwakani.

Kwa mujibu wa wakala wake, Bruno Satin, PSG ni moja kati ya klabu ambazo zinahitaji huduma yake na zinavutiwa kuanza mazungumzo na raia huyo wa Argentina.

Akizungumza na chanzo kimoja cha habari za michezo wakala wa mshambuliaji huyo alisema Aguero ndiye kipaumbele cha Pochettino ambaye amechukua nafasi ya Thomas Tuchel hivi karibuni.

PSG tayari wana namba nzuri ya washambuliaji wenye viwango bora kama Neymar, Kylian Mbappe, huku Lionel Messi akiwa anahusishwa kwa siku za hivi karibuni.

Aguero amekuwa na mwanzo mbaya wa msimu kwa kulazimika kucheza mechi tatu tu kwa sababu ya shida ya majeraha.

## KWA UFUPI

### OZIL SAFARI IMEIVA
KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil yupo kwenye mazungumzo ya kujiunga na klabu ya Uturuki ya Fenerbahce kwa mkopo kwa kipindi cha msimu kilichobaki. Hata hivyo, Washika Bunduki hao wamesema hawatalipa sehemu yoyote ya mshahara wake wa pauni 350,000 kwa wiki. (Guardian)

### ARSENAL YAMWANIA BRANDT
ARSENAL inahusishwa na kumwania winga wa Borussia Dortmund, Julian Brandt mwenye umri wa miaka 24, huku klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ikiwa tayari kumuuza nyota huyo. (Bild)

### MILITAO KUTUA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur inawania kumsajili mlinzi wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Brazil, Eder Militao mwenye umri wa miaka 22. (Mundo Deportivo)

### ALDERWEIRELD SOKONI
MLINZI wa kati wa Tottenham Hotspur, Toby Alderweireld mwenye umri wa miaka 31, anawaniwa na PSV Eindhoven. (De Telegraaf)

### VALENCIA YAMTAKA WINKS
KLABU ya Valencia imefanya mazungumzo na Tottenham juu ya kiungo wa England, Harry Winks, lakini wamekataa kufikia bei inayotakiwa na Spurs kwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 24. (AS)

### TRIPPIER APOTEZA
MLINZI wa Atletico Madrid, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 30, alikuwa anakaribia kutua Manchester United, lakini adhabu yake ya kufungiwa mechi 10 imeharibu dili hilo. (Talksport)

### ROMERO, ROJO 'OUT'
KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amesema golikipa, Sergio Romero mwenye umri wa miaka 33, na mlinzi Marcos Rojomwenye miaka 30, wanaweza kuondoka klabuni hapo mwezi huu. (Manchester Evening News)

### BERNARD KUUZWA
KLABU ya Everton ipo kwenye mazungumzo na Roma kuhusu kumuuza kiungo wa Brazil, Bernard mwenye umriwa miaka 28, amesema kocha wake, Carlo Ancelotti. (Liverpool Echo)

### WILLIAMS NJIA MOJA
MLINZI wa kushoto wa Manchester United, Brandon Williams atapenda kuondoka kwa mkopo kwenda kwenye klabu nyingine ya Ligi Kuu England, huku Newcastle United na Southampton zikihusishwa na nyota huyo mwenye umri wa miaka 20. (Manchester Evening News)

### BENKOVIC SOKONI
KLABU ya Celtic ipo kwenye mazungumzo na Leicester City kuhusu kumsajili mlinzi wa kati wa Croatia, Filip Benkovic. (Sky Sports)



HABARI MICHEZO

# CHAMA AFUNGUKA WAKO TAYARI KUPAMBANA CAF

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa kimataifa wa Simba Mzambia, Clatous Chama, amesema wachezaji wa timu hiyo wako tayari na kamili kupambana katika mechi za hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.

Chama ametoa kauli hiyo baada ya ratiba ya Kundi A kuonyesha Simba iko pamoja na vigogo Al Ahly ya Misri, AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Al Merreikh ya Sudan.

Kiungo huyo alisema katika soka la sasa hakuna timu nyepesi au ndogo na kinachotakiwa kutekelezwa ni kufanya maandalizi bora kuelekea michezo hiyo.

"Tuko tayari kuwakaribisha kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, tuko kamili," alisema kwa kifupi Mzambia huyo baada ya kufahamu wapinzani wa Simba kwenye hatua hiyo ya makundi.

Simba itacheza mechi yake ya kwanza kati ya Februari 12 na 13, mwaka huu dhidi ya AS Vita halafu itarejea nyumbani kuwakaribisha Al Ahly Februari 23, mwaka huu halafu itaelekea Khartoum kuwafuta Al Merreikh kati ya Machi 5 na 6 huku ikiwakaribisha Waarabu hao jijini Dar es Salaam Machi 16, mwaka huu.

Mechi yake ya tano itachezwa kati ya Aprili 2 na 3, mwaka huu nyumbani dhidi ya AS Vita na itamaliza hatua hiyo ya makundi kwa kuwafuata Al Ahly kati ya Aprili 9 na 10, mwaka huu.

Timu mbili zitakazofanya vyema kutoka katika kila kundi zitatinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayofanyika kila mwaka chini ya usimamizi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Wekundu wa Msimbazi walitinga hatua hiyo kwa kishindo baada ya kuwafunga wapinzani wao FC Platinum mabao 4-0 kwenye mchezo wa marudiano hapa jijini, wakati walilala goli 1-0 katika mechi ya kwanza iliyochezwa jijini Harare, Zimbabwe Desemba, mwaka jana.



Ofisa Uhusiano wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Najaha Bakari (katikati), akizungumza kuhusu maandalizi ya uchaguzi mkuu wa Shirikisho la Riadha Nchini (RT), unaotarajiwa kufanyika Januari 30, mwaka huu. Kushoto ni Makamu wa Rais wa shirikisho hilo, William Karage na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi, Dk. Jonas Tiboroha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# JKT Tanzania yasaka straika, beki

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha kikosi chake kinarejesha makali kwenye mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Mohammed Abdallah `Bares` amesema anahitaji kusajili wachezaji wawili wapya.

Bares aliliambia gazeti hili jana wachezaji anaowahitaji ili kuimarisha kikosi chake na ameainisha kwenye ripoti aliowakabidhi viongozi ni wa nafasi ya ulinzi na ushambuliaji.

Kocha huyo alisema idara hizo ndio zilionekana tatizo katika kikosi chake kwenye mechi za mzunguko wa kwanza na ili kufikia malengo yao anahitaji kusajili nyota hao wawili.

"Sasa hivi ni jukumu la viongozi kutekeleza, kwa sababu tayari nimeshawakabidhi majina, sio busara nikayataja kuhofia wachezaji hao bado wapo katika timu zao au kuna timu nyingine zinawahitaji, mambo yakiwa sawa tutaweka wazi," alisema Bares.

Aliongeza kazi yake kubwa ni kuhakikisha anafanikiwa kutimiza mipango yao kwa kumaliza ligi wakiwa ndani ya nafasi 10 za juu licha ya ushindani na ugumu uliopo kwenye ligi hiyo.

"Malengo yetu ni kuweka mambo yetu sawa ili kucheza soka la ushindani mkubwa kwa yoyote tutakayekutana naye katika ligi, tunataka kujiondoa kwenye presha ya kujinusuru kushuka daraja, tutoke mkiani mapema," alisema kocha huyo.

Kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara, JKT Tanzania iko katika nafasi 12 ikiwa na pointi 20 wakati vinara wa ligi hiyo ni Yanga wenye pointi 44 wakifuatiwa na mabingwa watetezi, Simba yenye pointi 35, lakini imecheza mechi tatu pungufu.

# CHANETA yawapigia magoti Ma-RC

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Netiboli Tanzania (CHANETA) kimewaomba wakuu wa mikoa kuvisaidia vyama vya mchezo huo katika kusimamia mashindano mbalimbali yanayofanyika mikoani humo.

Kauli hiyo imetolewa baada ya kumalizika kwa mashindano ya Kombe la Taifa yaliyofanyika Mjini Babati, mkoani Manyara hapo juzi.

Akizungumza na gazeti hili, Katibu Msaidizi wa CHANETA, Hilda Mwakatobe alisema wamelazimika kutoa kauli hiyo baada ya kuona timu nyingi zimeshindwa kushiriki kutokana na kukosa fedha.

Mwakatobe alisema hali hiyo ilifanya idadi ya timu shiriki katika mashindano hayo ipungue na hivyo kupunguza ushindani uliotarajiwa.

"Ninaomba wakuu wa mikoa pamoja na wilaya wazisaidie timu zao ili ziweze kushiriki mashindano ya Taifa, kiukweli viongozi wa mikoa peke yake hawawezi, wameyumba kiuchumi na wanahitaji msaada wa serikali na wadau," alisema Mwakatobe.

Alisema kati ya timu 26 zilizotakiwa kushiriki katika mashindano hayo, ni mikoa 11 tu ndiyo ilifanikiwa kuleta vikosi vyao kwenye michuano hiyo.

"Hata mkoa wa Dar es Salaam umetoa timu moja tu ya Ubungo, wilaya nyingine zote ambazo zimepewa hadhi ya mkoa hazijashiriki," Mwakatobe alisema.

Timu ya Mkoa wa Dodoma ndio ilifanikiwa kutwaa ubingwa wa michuano hiyo mwaka huu.

# Uchaguzi TTTA kufanyika Aprili

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Mchezo wa Meza Tanzania (TTTA), kinatarajia kufanya uchaguzi mkuu mapema Aprili, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Katibu Msaidizi wa TTTA, Leonard Liunda, alisema nafasi ambazo zitawaniwa katika uchaguzi wa chama hicho ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Mweka Hazina na Wajumbe wa Kamati ya Utendaji.


Liunda alisema maandalizi ya uchaguzi huo yameshaanza na wanawaomba wadau kujitokeza kuwania nafasi hizo ili kuongeza nguvu katika kuendeleza mchezo huo.

"Tunatarajia kufanya uchaguzi mkuu ifikapo Aprili, ninaimani tutapata viongozi ambao wataleta ushindani ndani ya chama chetu kwa ajili ya kuupa mafanikio mchezo huu," alisema Liunda.

Aliongeza uchaguzi huo utafanyika kwa kufuata mwongozo kutoka katika Baraza la Michezo la Taifa (BMT), ambao utasaidia kusimamia kanuni, taratibu na sheria za nchi.

"Awali tulipanga kufanya uchaguzi Desemba, mwaka jana, lakini tukaahirisha kwa sababu ya kusubiri mwongozo kutoka BMT (Baraza la Michezo la Taifa), lakini corona pia ilisababishwa kusimamisha mchakato," alisema kiongozi huyo.

Michezo
Jumapili Januari 10, 2021
Nipashe



## Pochettino amtaka Aguero atue PSG

HABARI UK 22

# Kaze aimwagia sifa Namungo

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema haikuwa kazi rahisi kwa timu yake kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Namungo katika mechi ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi kutokana na wapinzani hao kuwa na kikosi kizuri na kinachocheza soka safi.

Ushindi huo umeifanya Yanga kunusa hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo na itajulikana baada ya jana usiku kumalizika kwa michezo ya hatua ya makundi.

Kaze alisema kikosi cha Namungo kimeendelea kuwa imara na kucheza kwa kujiamini kutokana na kuwamo kwenye mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kocha huyo alisema wachezaji wake walicheza kwa presha kwa sababu walifahamu matokeo yoyote yale isipokuwa ushindi yangewaondoa kwenye michuano hiyo inayoendelea kwenye Uwanja wa Amaan Visiwani Zanzibar.

"Ulikuwa mchezo mgumu na tulikwenda kucheza na timu ambayo inajiamini kwa sababu ipo kwenye michuano ya kimataifa, lakini inacheza vizuri, hivyo haikuwa rahisi hata kidogo," alisema Kaze.

Aliongeza tatizo lingine liliwapa tabu Yanga ni kutumia wachezaji vijana na baadhi ambao hawajacheza muda mrefu, hivyo walikuwa wanashindwa kuhimili 'presha' ya mashabiki.

"Si rahisi sana kwa timu kama Yanga kuchezesha wachezaji wa aina hiyo, kwa sababu timu ikifungwa watu wanasema sana, lakini ndiyo inabidi baadhi ya wachezaji vijana nao wapate nafasi kwa ajili ya kupata uzoefu," Kaze aliongeza.

Naye Kocha Mkuu wa Namungo, Hemed Suleiman Morocco alisema wamepoteza mechi hiyo baada ya wachezaji wake kutokuwa makini hasa mwanzoni mwa mchezo huo.

"Tumeanza kucheza vizuri na kuikamata mechi baada ya kufungwa. Tulianza kwa tahadhari na kwa kuzuia kwa sababu tulijua Yanga watakuja kwa nguvu kwenye dakika za mwanzo kwa sababu walipoteza mechi ya kwanza," alisema kiungo huyo wa zamani wa Coastal Union na Timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes).

HUPITI HAPA



Mshambuliaji wa Yanga, Yacouba Songne (kulia), akijiandaa kumtoka mchezaji wa Namungo FC katika mechi ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi iliyochezwa juzi usiku. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# MAKOCHA WAZUNGU WAIGOMBEA SIMBA

## Uongozi wasema umepokea maombi zaidi ya 100 wakitaka kurithi mikoba...

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA ni siku nne zimepita tangu aliyekuwa Kocha Mkuu, Sven Vandenbroeck, atangaze kubwaga manyanga kuwafundisha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, zaidi ya makocha 100 kutoka sehemu mbalimbali duniani wametuma maombi kutaka kurithi mikoba ya Mbelgiji huyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, kiongozi mmoja wa juu wa Simba alisema uongozi wa timu hiyo hautafanya haraka kuteua kocha mpya kwa sababu inahitaji kuendelea kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu Bara na kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika mashindano ya kimataifa.

Kiongozi huyo alisema dalili za makocha wengi kuomba kazi ya kuifundisha Simba ni nzuri, kwa sababu klabu hiyo inaelekea kutimiza malengo yake ya kuwa moja ya vigogo wa Afrika.

Chanzo hicho kiliongeza uamuzi wa kumpata mrithi wa Sven utatekelezwa baada ya kupitia rekodi za makocha hao walioomba na wale ambao Simba imewafuata kutokana na mafanikio waliyowahi kupata huko nyuma.

"Simba imeshakuwa 'brand kubwa', yaani ndani ya siku mbili (juzi), tulikuwa tumeshapokea maombi zaidi ya 100, tena wengi ni Wazungu, ila tunaahidi tutafanya umakini katika kupata kocha mpya," kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza klabu hiyo imeshakuwa na hadhi kubwa, hivyo wanahitaji kocha ambaye ataivusha na kuipeleka kule ambako haijafika kwa muda mrefu.

"Hatuangalii makundi, sasa hivi tunaangalia robo fainali ya Afrika na tukifika hapo, watatujua sisi ni Simba kweli, hadi wiki ijayo atajulikana kocha anayekuja, tumejipanga kuwashangaza," kiliongeza chanzo hicho.

**WEILER APEWA NAFASI**

Kocha wa zamani wa Al Ahly, Rene Weiler, ambaye ni raia wa Uswisi anatajwa kuwa na nafasi kubwa ya kutangazwa kutua nchini kuwaongoza wawakilishi hao pekee wa Tanzania katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Weiler ambaye alitangaza kustaafu kucheza soka la ushindani mwaka 2001, amekuwa huru tangu Oktoba, mwaka jana.

Sven aliamua kuachana na Simba ikiwa ni muda mfupi baada ya kuipa kichapo cha mabao 4-0 FC Platinum ya Zimbabwe na kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa ushindi wa jumla wa mabao 4-1.

Uongozi wa Simba umetangaza kikosi chao ambacho kwa sasa kiko kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar, kitakuwa chini ya Suleiman Matola na jana usiku kilitarajiwa kuwakabili Mtibwa Sugar katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi.

9 770856 541002 >
GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042